tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

**Mshtakiwa** adai hajui kosa lake, awasilisha kilio kwa wanahabari

UKURASA 4




UKURASA 11

Nipashe
Jumatatu Septemba 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581430
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Adaiwa kusota gerezani kwa miaka 10 bila kesi

• **Mahakama** yasema haihusiki, DPP, Magereza...

*Endelea ukurasa 2*



Kamishna Jenerali wa Magereza, Mzee Ramadhan Nyamka

Mkurugenzi wa Mashtaka, Sylvester Mwakitalu

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

MATUKIO YA KUJIUA

**WASIO NA KAZI, WANACHUO HATARINI AFYA YA AKILI**

HISTORIA ya familia kuwapo matukio ya mmoja wa wanafamilia aliyewahi kujinyonga, matumizi ya vilevi, mabadiliko...

UKURASA WA 5

**VIGOGO CCM WAZINDUA KAMPENI MBARALI**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimezindua kampeni zake katika Jimbo la Mbarali, huku mgombea anayewania...

UKURASA WA 8

**DK. MWINYI APONGEZA CRDB KWA HUDUMA KUZINGATIA IMANI YA DINI**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Benki ya CRDB kwa...

## Hadhari yatolewa kwa wanaofanya ‘doria’ katika simu za wenza wao

UKURASA 16



## Lissu, wenzake wakamatwa hotelini

• **Mbowe:** Tuna hofu na usalama wao... *Endelea ukurasa 3*

**MICHEZO** **AUBIN KRAMO AMUIBUA ROBERTINHO** UK.24

**KATUNI** UK.6

RIPOTI MAALUM

# Adaiwa kusota gerezani kwa miaka 10 bila kesi

**Na Mwandishi Wetu**



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni

JOHN Robert Maitland anadaiwa kusota mahabusu gerezani nchini kwa zaidi ya miaka 10 bila kosa. Uongozi wa Mahakama umesema hana kesi inayomkabili na haihusiki na kushikiliwa kwake.

Udadisi wa Nipashe kuhusu suala hilo umebaini kuwa awali Maitland, alikuwa anakabiliwa na mashtaka ya kuingia na kuishi nchini kinyume cha sheria. Alituhumiwa kuwa na uraia wa Tanzania, Uingereza na Afrika Kusini.

Ndugu wa mahabusu huyo, Kenan Makweta, aliiambia Nipashe jijini Dar es Salaam kuwa Maitland alikamatwa na Idara ya Uhamiaji Januari 8, 2010, kijijini kwake Muleba na kufikishwa Mahakama ya Wilaya ya Bukoba.

Alidai kuwa tangu kipindi hicho, ndugu yake huyo alikuwa anakamatwa na kuwekwa mahabusu kwa muda na kisha kuachiwa.

Msaidizi wa Msajili wa Mahakama ya Tanzania, Jovine Bishanga, aliiambia Nipashe mwishoni mwa wiki kwamba, mtuhumiwa huyo hana kesi mahakamani na wao hawahusiki na kushikiliwa kwake.

Alidai kuwa Mahakama ya Wilaya ya Bukoba ilimhukumu Februari 24, 2010 kutumikia kifungo cha miaka miwili gerezani na kulipa faini ya Sh. 80,000. Alikata rufani Mahakama Kuu ambayo ilikazia hukumu ya miaka miwili na kuondoa faini.

Rufani hiyo ni namba 9/2011 katika Mahakama Kuu ya Tanzania. Ingawa Bishanga hakutaja ni linI Maitland alitolewa gerezani, taarifa za mahakama zinaonesha kwamba Januari 13, 2011, alirudishwa tena gerezani kwa tuhuma za uraia.

"Januari 17, 2011 alifungwa kutumikia kifungo cha miezi sita na viboko 10 kwa kosa la kuidharau mahakama kwa rufani namba 9/2011 H/C (T) Bukoba na kumaliza kifungo hicho Septemba 3, 2011," inaeleza taarifa ya mahakama.

Baada ya kumaliza adhabu hiyo, Maitland hakuachiwa kutokana na kesi ya kuingia na kuishi nchini kinyume cha sheria iliyokuwa Mahakama ya Wilaya ya Bukoba.

Bila kueleza aliachiliwa mara ngapi, Bishanga alisema Maitland amekuwa akiondolewa gerezani kwa hati ya kuondoshwa.

Bila kueleza alikaa uraiani au magereza kwa muda gani, Bishanga alisema Maitland alikamatwa wilayani Muleba Januari 7, 2013 na kuwekwa mahabusu hadi sasa.

"Toka wakati huo, aliwekwa kizuizini katika Gereza la Bukoba kwa amri ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi hadi Mei 17, 2022 alipoletwa Gereza la Segerea," alisema.

Taarifa zinaonesha kwamba Maitland aliwahi kuondolewa gerezani kwa hati ya kuondoshwa (remove order), Machi Mosi, 2019.

**NDUGU WALALAMA**

Makweta aliyewasilisha malalamiko yao dhidi ya kinachoendelea kwa ndugu yao, alidai kuwa Maitland alikata rufani namba 179/2011 katika Mahakama ya Rufani ambayo nayo Juni 4, 2012 ilikazia hukumu ya miaka miwili gerezani.

Alidai Desemba 4, 2012 Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alitoa kibali cha kuondolewa nchini kwa mahabusu huyo; na mwezi mmoja baadaye, Januari 7, 2013, alikamatwa na kupelekwa gerezani Bukoba kisha kuhamishiwa Gereza la Segerea, jijini Dar es Salaam aliko hadi sasa.

Wakati hayo yanajiri, Makweta alidai Maitland anaendelea kusisitiza kuwa ni mzaliwa wa Buguma, Muleba mkoani Kagera kwa baba na mama yake, ambao wote ni Watanzania.

Makweta alidai ndugu yake huyo alizaliwa mwaka 1968 katika eneo la Buguma, wazazi wake wakiwa ni wakulima wa kahawa, kilimo kilichokuwa kinaendelezwa na mtuhumiwa huyo hadi alipokamatwa.

"Kwa zaidi ya miaka 10 sasa, Robert yuko mahabusu na kibaya zaidi ni kwamba hapelekwi mahakamani, badala yake anashauriwa achague nchi ya kwenda ndipo ataachiwa huru, vinginevyo ataendelea kukaa gerezani," alidai.

Makweta alidai kuwa baada ya kukosa haki ndani ya nchi, Maitland alifungua shauri katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, ambayo ilizisikiliza pande zote ikiwamo Serikali ya Tanzania. Alishinda.

Katika hukumu ya kesi hiyo ambayo Nipashe imeona nakala yake, jopo la Tanzania liliongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Masuala ya Katiba na Haki za Binadamu, Sarah Mwaipopo, aliyeambatana na Mkuu wa Kitengo cha Sheria katika Wizara ya Mambo ya Nje, Baraka Luvanda na Mkurugenzi Msaidizi Haki za Binadamu na Wakili Mkuu wa Serikali, Nkasori Sarakikya.

Wengine ni Wakili wa Serikali Mwandamizi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Richard Kilanga na Ofisa Sheria kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, Blandina Kasagama.

Maitland aliwakilishwa na Wakili Peres Seneto Parpai wa Star Attorney Chamber, na bibi yake aitwaye, Georgia Pennesis.

Katika shauri hilo namba 013/2015, Tanzania ilitakiwa kuthibitisha madai ya uraia wa Maitland ambayo yalimtia hatiani katika mahakama za Tanzania.

Tanzania ilidai Maitland ana uraia pacha wa Uingereza na Afrika Kusini, tuhuma ambazo hazikuthibitishwa kwa vielelezo kama agizo la mahakama hiyo lilivyotaka.

Badala yake, Tanzania iliwasilisha madai 12 mahakamani hapo kuwa mahakama za Tanzania ikiwamo ya rufani zimethibitisha kwamba Maitland si Mtanzania, bali ana uraia pacha kinyume cha Sheria ya Uraia inayozuia uraia pacha.

Ilidaiwa Maitland hakuwahi kuwa raia wa Tanzania. Ameshikiliwa kihalali na kuomba shauri hilo litupiliwe mbali.

Maitland aliwasilisha cheti chake cha kuzaliwa namba 00001642 na hati ya dharura ya kusafiria iliyotolewa na mamlaka za Tanzania.

Mama mzazi wa mtuhumiwa huyo, Anastasia Pennesis, ambaye ni raia wa Tanzania mwenye hati ya kusafiria namba AB316143, alifika mahakamani huko na kuthibitisha mwanawe ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa.

Hukumu ya kesi hiyo ilitolewa Novemba 28, 2019 katika kikao cha kawaida cha mahakama hiyo kilichoketi visiwani Zanzibar, chini ya Rais wake, Sylvain Ore, Makamu wake, Ben Kioko na majaji Gerard Niyungeko, El Hadji Guisse, Rafaa Ben Achour, Angelo Matusse, Tujilane Chizumila, Chafika Bensaoula na Msajili wa Mahakama hiyo, Robert Eno.

**DPP, MAGEREZA**

Mwandishi wa habari hizi, katika kusaka ufafanuzi wa mamlaka za serikali, aliwasiliana na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Sylester Mwakitalu, Agosti 24, 2023 ambaye aliahidi kufuatilia ili kujua sababu za Maitland kukaa mahabusu bila kupelekwa mahakamani.

DPP Mwakitalu aliahidi kutoa ufafanuzi siku tatu baadaye, lakini kwa zaidi ya wiki mbili sasa hatoi ushirikiano kwa mwandishi.

Msajili wa Mahakama, Wilbert Chuma, aliulizwa na mwandishi kuhusu suala hilo, alimwelekeza msaidizi wake, Jovine Bishanga, kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko ya mahabusu huyo.

Agosti 25, 2023, mwandishi alikwenda Gereza la Segerea na kuonana na Mkuu wa Gereza, Hamisi Lissu, ambaye alikataa kuzungumzia suala hilo kwa maelezo "wakubwa wote wanalifahamu".

"Mtafute Kamishna Mkuu wa Magereza, yeye atakupa ufafanuzi. Mimi si Msemaji wa (Jeshi la) Magereza," alisema.

Mwandishi alipohitaji ufafanuzi toka kwa Mkuu wa Idara ya Habari ya Magereza, Juma Kapilima, alimtaka awasiliane na Mkuu wa Gereza la Segerea.

"Hilo anaweza kulifafanua Mkuu wa Gereza, lakini acha na mimi nifuatilie nitafute kesho," alisema.

Hata hivyo, Kapilima alipotafutwa siku iliyofuata, alidai hakuwa amepata taarifa za kina kuhusu mahabusu huyo.

# Lissu, wenzake wakamatwa hotelini Mbowe: Tuna hofu na usalama wao

**Na Mwandishi Wetu,**
KARATU

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Tundu Lissu, amekamatwa na kushikiliwa na makachero wa Jeshi la Polisi akiwa hotelini wilayani Karatu, mkoani Arusha.

Inadaiwa Lissu amekamatwa pamoja na Katibu wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA), Catherine Ruge.

Lissu na msafara wake walikuwa katika mwendelezo wa 'Operesheni +255, Katiba Mpya, Okoa Bandari Zetu'.

Kabla ya kutiwa nguvuni, majira ya saa 4:00 asubuhi, makachero hao wanadaiwa walifika katika Hoteli ya Ngorongoro iliyoko Karatu na kuizingira wakiwa na mitutu ya bunduki na mabomu.

Baadhi ya watu waliokuwa katika msafara huo, wamedai kuwa jeshi hilo liliwaeleza watoa huduma wa hoteli hiyo kwamba wanataka kujua chumba alimokuwa amelala Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Lissu. Walielezwa na kwenda chumbani.

Inadaiwa kuwa baada ya askari wa Jeshi la Polisi kuingia katika chumba hicho, walimchukua Lissu na kuondoka naye bila kumweleza walikotaka kumpeleka.

Wengine wanaodaiwa kukamatwa na Jeshi hilo ni Susan Kiwanga, Mjumbe wa Kamati Kuu, Catherine Ruge, ambaye ni Katibu BAWACHA Taifa, Twaha Mwaipaya, walinzi wa Lissu pamoja na na watu wengine ambao majina hayo hayajatajwa.

Ijumaa iliyopita, Lissu alifanikiwa kuingia wilayani Ngorongoro na kupata mapokezi makubwa. Alifanya mkutano katika Kijiji cha Ololosokwani licha ya kuwapo zuio la Jeshi la Polisi.

Jumamosi, Lissu na ujumbe wake walitarajiwa kufanya mikutano katika Tarafa za Loliondo na Ngorongoro, lakini hawakufanikiwa kutokana na upinzani wa polisi waliomzuia kufanya mikutano.

Kutokana na zuio hilo, Lissu alilazimika kutumia njia nyingine ya kuzungumza na wafugaji wa jamii ya Kimasai katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) kwa kutumia simu yake ya mkononi.

Jana, Lissu alitarajiwa kufanya mkutano mwingine katika Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha.

**MBOWE ALAANI**

Kupitia ukurasa wake wa Twitter jana, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, aliandika: "Tunalaani ukamataji, unyanyasaji, usumbufu unaofanywa na Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola kwa Makamu Mwenyekiti wa chama chetu, Mheshimiwa Tundu Lissu na viongozi wengine waandamizi wa ngazi mbalimbali, wanachama na wapenzi wetu huko mkoani Arusha.

"Kwa uzito huohuo, tunalaani uzuiaji wa mikutano yetu na shughuli halali za kisiasa huko Ngorongoro, Loliondo na Karatu. Tuna hofu kubwa ya usalama wa watu wetu, na ni dhahiri sasa serikali inarejesha utawala wa mabavu usiothamini haki, uhuru na demokrasia.

"Tunafuatulia kwa karibu na tunadai kuachiliwa haraka na bila masharti kwa watu wetu wote."

**KAULI YA POLISI**

Jana Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, lilithibitisha kumshikilia Lissu na wenzake watatu kwa ajili ya mahojiano kuhusiana na tuhuma za kufanya mikusanyiko isiyo halali na kuwazuia askari polisi kutekeleza majukumu yao.

Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Kamishna Msaidizi Justine Masejo, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, alisema kuwa baada ya mahojiano hayo na ukamilishwaji wa taratibu zingine, hatua nyingine za kisheria zitafuatwa.



Watoto wenye ulemavu wa viungo Rehema John (Kulia) mkazi wa kijiji cha Mabovu kata ya Kwafungo na mtoto Fatuma Mohamed (Kushoto) mkazi wa kijiji cha Mkuzi Wilayani Muheza Tanga wakikabidhiwa msaada wa viti vya matairi matatu na viongozi wa Taasisi ya Jamiyatul Akhlaaqul Islam (JAI) wilayani hapa mwishoni mwa wiki ambao umetolewa na mfadhili kutoka mkoani Lindi. **PICHA:MPIGAPICHA WETU.**

MATUKIO YA KUJIUA

# Wasio na kazi, wanachuo hatarini afya ya akili

## •Wamo walioachika, kila mwaka watu 700,000 hujiua

**Na Christina Mwakangale**

HISTORIA ya familia kuwapo matukio ya mmoja wa wanafamilia aliyewahi kujinyonga, matumizi ya vilevi, mabadiliko ya ghafla maishani kama vile usaliti na mihemko, imehusishwa na mazingira ya moja kwa moja ya mtu kujikatisha uhai.

Licha ya wanaume kuwa vinara kutenda vitendo hivyo, wataalamu wametaja kundi hatarishi linaloweza kujikatisha uhai, linajumuisha wasio na kazi (jobless), waleapekee (singles), walio na uhusiano ama wanandoa na watalaka.

Mabingwa wa Afya ya Akili kwa nyakati tofauti wamebainisha hayo katika maadhimisho Siku ya Kuongeza Uelewa na elimu katika kuzuia visa vya watu kujikatisha maisha ama kujiua duniani, iliyoadhimishwa jana. Kitaifa iliadhimishwa jijini Dodoma.

Bingwa wa Afya ya Akili kutoka Idara ya Afya ya Akili Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Dk. Raymond Mgeni, alisema kuwa Septemba 10 kila mwaka ni siku maalum kwa ajili ya kuongeza uelewa. Visa vya kujikatisha maisha zaidi hutokea kwa wanaume.

"Nimekutana na kisa ambacho mgonjwa wangu licha ya kwamba niliongea naye, ila nikapata taarifa kajinyonga. Kila mwaka kuna visa karibu 700,000 hutokea kwa watu kujikatisha maisha.

"Unapokuja katika uwiano, basi visa vingi ni vya wanaume, kwa maana kutimiza adhma ya kujiua hadi kukamilika. Hii huchangiwa na aina ya mbinu wanazotumia kujiondoa uhai mbali na ilivyo kwa wanawake," alifafanua.

Bingwa huyo alisema sababu ya wanaume kufanya vitendo hivyo ni kutokuwa wepesi kueleza mambo yao yanayowakabili, hivyo hufikia ngazi hiyo kimyakimya, bila hata wengine kugundua.

"Njia wanazotumia kujiua huwa zina nafasi ndogo kupona. Mfano, kujipiga risasi, kujirusha katika majengo marefu, kujikata shingo, kunywa sumu kali, hasa dawa za mashambani.

"Hii ya kunywa sumu kali kwa mwaka huu hospitalini petu (MZRH) tumepata visa vinne kuanzia Januari hadi Agosti," alibainisha Dk. Raymond.

Akiyataja mazingira husianishi yanayoweza kuchangia vitendo hivyo, Dk. Raymond alisema ni kuwapo historia ya mwanafamilia kujinyonga, matumizi ya vilevi kama pombe, dawa za kulevya, bangi, usaliti na haiba fulani.

"Hayo ni mazingira husianishi. Hapo ujue mtu yupo katika hali ya mgogoro mkubwa katika nafsi. Haianzi moja kwa moja ghafla tu. Nia kusudio, mawazo ya kujidhuru, mipango, jaribio kisha kutumia nia ya kujiua, ni mipango anayoipanga mtekelezaji mapema.

"Mgogoro wa nafsi na akili huwa mkubwa kiasi kwamba unalowazia lililo na nafuu ni kujiondosha uhai. Hana tumaini. Ila inawezekana kusaidia, ingawa wengine licha kushauriwa huwa hawaachi kuendelea kupanga mpango wa kujiua," alisema bingwa huyo.

Alifafanua kwamba, baadhi hujiua endapo wanapata dalili ya ugonjwa wa akili wa kusikia sauti amrishi akilini, ambazo zinaambatana na sauti za kumwarisha eneo lolote iwe mazingira ya starehe au nyumbani.

"Upo baa unapata moja mbili tatu, halafu unaingia ugomvi wa kurushiana maneno na mtu jirani yako. Halafu una cha moto ghafla unapata jazba, unaamua kutoa na kufyatua.

"Umefyatua ghafla, unatambua itakuwa umeua. Basi unasema bora nijimalizie tu, unageuza cha moto unaelekeza kwenye kichwa.

"Mihemko usiyojua matokeo yake ni mojawapo ya mazingira hatari sana. Ila kuna kundi lililopo hatarini zaidi ya kujiondoa uhai. Mfano, wasio na kazi (jobless), waleapekee (singles), walio na uhusiano ama wanandoa na watalaka.

"Kuhusishwa makundi hayo, haina maana ukiwa 'single' utajinyonga, au ukiwa umepata 'breakups' (umetengana na mtu wako). Ila imewekwa uhusiano wa kutokea ni kubwa. Huku kesi nyingi tunaziona kwa vijana rika na wanachuo.

"Kama imetokea uhusiano yamevunjika, biashara imefilisika, basi kubaliana na huo uhalisia na kuchukua hatua inayofuata.

"Huu ni ujuzi ambao ni muhimu kufahamu ili mambo yanapojitokeza ghafla, tuwe tayari kukubaliana nayo. Watu wanakosa kukabiliana na kukubali kuchukua hatua mpya, kusonga mbele," alishauri.

Bingwa Mwandamizi wa Afya na Magonjwa ya Akili Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Afya ya Akili Tanzania (MEHATA), Dk. Saidi Kuganda, alisema dhana tofauti katika jamii zinazoongozwa na malezi na hamasa za kijinsia, ni miongoni mwa sababu zinazofanya baadhi ya wanaume kujiona wanyonge.

"Siku hizi hata wanawake ni majasiri. Wanaume ndio wameanza kuwa wanyonge. Pia, matukio hayo ni hitilafu katika akili na uwezo wa kuamua jambo sahihi kwa wakati sahihi.

"Nilitembelea shule moja hapa mkoani kubaini changamoto za wavulana. Kwa pamoja wamelalamika kuwa wasichana wamekuwa wanapewa kipaumbele, hamasa na kutambuliwa kwa kila wanachofanya, lakini kamwe si kwao, matokeo yake wameanza kuwa wakaidi, wapweke.

"Sasa hizo changamoto, unyonge, kuona hawezi kumwambia mtu kitu, zikikutana na haya mambo ndipo mlipuko unapotokea. Kwa asilimia 100 binadamu ni uhusiano wa kijamii. Jambo linakushinda mpatie mwenzio. Upweke huua," alionya bingwa huyo.

**KUPOTEA KWA CHETI**



**INVIOLATA MICHAEL MNYINGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0806-0032** kilichotolewa na CITY SECONDARY SCHOOL mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/8651/2023.**

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Mshtakiwa adai hajui kosa lake

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Revocatus Muyela anayeshtakiwa kumuua dada wa marehemu Erasto Msuya, maarufu Bilionea Msuya, Aneth Msuya, amedai anateseka gerezani kwa kosa ambalo halijui.

Muyela na aliyekuwa mke wa Bilionea Msuya, Miriam Mrita, wanashtakiwa kwa mauaji ya Aneth Msuya, aliyeuawa nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam Mei 25, 2016.

Mshtakiwa huyo alidai hayo mwishoni mwa wiki wakati akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza alipokuwa anasindikizwa kupanda basi kurudi mahabusu Segerea baada ya kesi yao kuahirisha.

"Waandishi wa habari mnaona yanayoendelea mahakamani. Ninateseka kwa kosa ambalo silijui ila Mungu atasimama. Mimi ni kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)," alidai Muyela.

Mshtakiwa huyo alidai hayo kutokana na ubishani wa kisheria uliokuwa umetokea ndani ya chumba cha mahakama kuhusiana na Taarifa ya Awali ya Siri ya Jeshi la Polisi (First Crime Report) ya tukio hilo la mauaji hayo.

Kesi hiyo inasikilizwa mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam. Leo, Shahidi wa 23, Sajenti Obadia Mwarukuta, ataendelea kuulizwa maswali ya dodoso na Mawakili wa Utetezi, Peter Kibatala na Nehemiah Nkoko.

Sajenti Mwarukuta katika ushahidi wake, alieleza utofauti wa vielelezo vya mahakama viliyoletwa na Upande wa Utetezi na Upande wa Jamhuri ambavyo vyoye vilikuwa ni taarifa ya siri ya jeshi hilo kuhusu tukio moja.

Shahidi huyo ambaye ni Ofisa wa Polisi kutoka Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai mkoani Dodoma, alidai kuwa taarifa hizo zina utofauti kwa kuwa ya Upande wa Utetezi ni nakala na ya Jamhuri ni halisi.

Alidai kuwa mwaka 2016 alikuwa Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai mkoani Dar es Salaam Kitengo cha Kumbukumbu cha Makosa ya Jinai na kwa sasa yuko Kitengo cha Kupambana na Dawa za Kulevya mkoani Dodoma.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, Sajenti Mwarukuta, alidai kuwa Mei 30, 2016, aliingia kazini. Wakati anaendelea na kazi zake zingine alizopangiwa, kuna nyaraka alizipokea kutoka Mkoa wa Kipolisi Temeke zinazohusiana na jinai.

"Hizi nyaraka mbili nikizingalia DE III ni nakala na hii PE 17 ni nyaraka halisi. Kwa uhalisia hazifanani. Nikiangalia eneo la juu ya hizi nyaraka, kuna utofauti kwa jinsi zilivyojazwa," alidai Sajenti Mwarukuta.

Shahidi aliendelea kudai kuwa kielelezo PE 17 kwenye namba ya upelelezi ya RCO ilipoandikwa ipo chini ya neno confidential (siri), ndipo linapotakiwa iandikwe.



Ofisa Tarafa ya Kwekivu,Wilaya ya Kilindi,Mkoa wa Tanga, Michael John akiteta jambo na wananchi waliofika kupata huduma za afya katika Zahanati ya kijiji cha Lumotio jana alitaka kujua jinsi watu wanavyohudumiwa hapo na wataalamu. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Wananchi watolewa hofu majibu ya vipimo vya DNA

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imewataka wananchi kutotilia shaka majibu ya vinasaba (DNA) yanayotolewa na wataalamu wake.

Uongozi wa mamlaka hiyo umesema upokeaji sampuli, upimaji na utoaji matokeo una mlolongo wa usiri na usiohusisha mtu mmoja.

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti katika mamlaka hiyo, Daniel Ndiyo, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki mjini Morogoro, alipomwakilisha Mkemia Mkuu wa Serikali kuzungumza na wataalamu wanaohusika na upokeaji, uchukuaji na mashauri yanayohusisha vipimo vya vinasaba, wanaopitia sheria inayohusika na suala hilo.

Akizungumza na wataalamu hao wakiwamo mahakimu, wataalamu wa maabara, waendesha mashtaka, maofisa upelelezi wa polisi, waendesha mashtaka na maofisa ustawi wa jamii mjini Morogoro, Ndiyo alisema upimaji DNA kwa sasa umekuwa wa kueleweka.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi na wataalamu juu ya teknolojia ya upimaji hali iliyosaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa malalamiko tofauti na zamani.

Alisema kwa sasa suala la vipimo vya DNA limeendelea kueleweka katika jamii. Sheria inayosimamia suala hilo inaangalia uchunguzi wa vinasaba vya binadamu na kulinda taarifa zinazotokana na uchunguzi unaofanyika.

"Teknolojia hii imekuwa inasaidia masuala kadhaa kama panapotokea janga la watu kutotambulika kwa ajali za kuungua moto ama kufariki dunia kwa maji kwa kuwa teknolojia hii inasaidia kutambua wahusika ni kina nani ili ndugu zao wawahifadhi kwa kuzingatia mila na desturi zao," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema faida nyingine ya teknolojia hiyo inayotumika katika maeneo mbalimbali, ni pamoja na kutibu changamoto mbalimbali za kiafya ikiwamo ugonjwa wa figo, jinsi tata kwa wale wenye jinsi mbili, uchunguzi wa usalama na ubora wa maji katika tiba ya figo na utambuzi wa uhalali wa watoto kwa wazazi. Unasaidia atika masuala ya mirathi.

Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Amina Mhando, alisema wamekuwa wanakutana na kesi ambazo mzazi anaweza kuwa anatunza mtoto, lakini hana uhakika kama ni mwanawe, hivyo kupewa utaratibu wa vipimo na wao huandika barua mahakamani kuomba ridhaa kufanyiwa vipimo.

"Mara nyingi sababu za kupima vinasaba ni kutokana na matunzo ya watoto na wengine hukwepa kutunza mtoto kwa kuhisi si mtoto wake.

"Kwa mwezi tumekuwa tunapokea karibu kesi 40 hadi 50 kwa Manispaa ya Morogoro ambazo nyingi ni matunzo ya watoto na migogoro ya familia," alisema Mhando.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Nanguji, Manispaa ya Morogoro, Dk. Salehe Nyumba, alisema taaluma ya vinasaba inasaidia kutatua changamoto kwenye jamii ikiwamo tatizo la ubakaji ambalo kwa sasa limeshika kasi.

Alitoa wito kwa jamii, wazazi na walezi kuhakikisha wanawafikisha kwa wakati hospitalini watu wanaofanyiwa vitendo hivyo. Wasioge wanapofanyiwa ukatili huo. Pia wasijisafishe wala kubadili mavazi waliyokuwa wamevaa.

Hakimu Mkazi Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Richard Kasele alisema kesi nyingi zinazohusu makosa ya jinai kama dawa za kulevya, mauaji na nyinginezo, wamekuwa wakihitaji vipimo vya vinasaba. Hupokea matokeo kutoka Jeshi la Polisi na hospitalini kulingana na shauri husika.

"Pia, kuna kesi tuliwahi kupokea ya ubakaji. Mtu mzima alituhumiwa kubaka, lakini katika mahakama kutaka kujiridhisha baada ya ushahidi, ililazimika kumpima mshtakiwa na ilibainika hakuwa na uwezo wa kufanya kitendo kile. Kumbe alisingiziwa.

"Bila DNA huenda ungetumika ushahidi wa kimazingira na mtuhumiwa angetiwa hatiani. Teknolojia mpya zimerahisisha sana," alisema hakimu huyo.

Vipimo vya DNA vilisaidia pia wakati wa tukio la moto ulioosababishwa na kulipuka lori la mafuta Agosti 10, 2019 maeneo ya Msamvu, mjini hapa ambako zaidi ya watu 60 walifariki dunia papo hapo kwa kuteketea kwa moto na walitambuliwa na ndugu zao kwa mfumo wa upimaji wa vinasaba, yaani DNA.

## Ng'ombe 38 wakamatwa wakipelekwa nje ya nchi

**Na Renatha Msungu**

JESHI la Polisi kupitia Kikosi cha Kupambana na Kuzuia Wizi wa Mifugo nchini, limekamata ng'ombe 38 waliokuwa wanatoroshwa kwenda nchi jirani huku likisisitiza wafugaji kuacha tabia hiyo. Wafuate sheria.

Mbali na hilo, jeshi hilo pia limeendelea kutoa elimu kwa wafugaji na makundi mengine ya wananchi kuhusu hasara za utoroshaji mifugo, likiwataka kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo dhidi ya wanaotorosha mifugo.

Taarifa iliyotolewa mwishoni mwa wiki na Kamanda wa Polisi wa Kikosi hicho nchini, Kamishna Msaidizi wa Polisi Simon Pasua, alibainisha kuwa kikosi hicho kimefanikiwa kukamata mifugo 38 na watuhumiwa waliokuwa wanatorosha mifugo hiyo kwenda nchi jirani.

"Tumefanikiwa kuwakamata watuhumiwa waliofanya kosa hilo. Tunaomba wananchi waendelee kutoa ushirikiano ili watuhumiwa wa aina hiyo wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria," alisema Kamanda Pasua.

Alisema kutokana na elimu inayotolewa na kikosi hicho kwa wafugaji, idadi ya mifugo inayoingia katika machinjio ya kimataifa ya Kiwanda cha Elia Food kilichoko Namanga wilayani ya Longido, mkoani Arusha imeongezeka.

Alisema wafugaji wanapaswa kutimiza matakwa ya sheria katika sekta ya mifugo katika kuisafirisha kwenda nje ya nchi badala ya kutorosha kama walivyofanya watuhumiwa hao ambao hakuwataja kwa majina.

Kamanda Pasua alisisitiza jamii iendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kuhakikisha mifugo inayosafirishwa kwenda nje, inasafirishwa kihalali na si vinginevyo.

Alisema jeshi hilo litaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na umuhimu wa kutoa taarifa kuhusu watuhumiwa wa utoroshaji mifugo kwenda nchi jirani bila kufuata sheria.

Kamanda Pasua pia alitoa wito kwa wananchi kuendelea kuwa wazalendo kwa kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi juu ya watu wanaache wanajihusisha na utoroshaji wa mifugo nchini na kuongeza kuwa wakifanya hivyo, watakuwa wamelisaidia taifa na kwamba hatua kali zitaendelea kuchukuliwa.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa ajivunia utekelezaji miradi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wananchi waendelee kumwamini Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa ana dhamira na malengo makubwa ya kuendelea kuboresha maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi.

"Tujenge imani ya serikali yetu, tujenge imani na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa anatupenda na amedhamiria kutuletea maendeleo.

"Hapa katika Kata ya Nanganga tumejengewa shule ya sekondari iliyogharimu Sh. milioni 470, watoto wanasoma," Majaliwa alisema jana alipozungumza na wananchi katika vijiji vya Mbecha, Nangumbu, Chimbila na Michenga akiwa katika ziara ya kukagua maendeleo wilayani Ruangwa.

Waziri Mkuu alisema serikali imeidhinisha fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo zikiwamo Sh. bilioni 169 kujenga mradi wa maji wa Nyangao-Ruangwa ambao utanufaisha wananchi katika vijiji 34 vya Ruangwa na 12 vya Nachingwea.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wanaoishi katika vijiji hivyo pamoja na vijiji vyote ambavyo mradi huo utapita. Wananchi waendelee kuwa na subira na imani na serikali yao.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wilaya hiyo inakuwa na miundombinu bora ya barabara, serikali imeridhia kutoa Sh. bilioni 69 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Nanganga-Ruangwa kwa kiwango cha lami.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema serikali imefanya maboresho makubwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi kwa kufunga mashine ya CT Scan iliyogharimu Sh. bilioni mbili, hivyo imewapunguzia wananchi safari ya kwenda Dar es Salaam kufuata kipimo hicho.

Alisema mbali na maboresho hayo, Hospitali ya Kanda ya Kusini iliyoko mkoani Mtwara, pia imeanza kutoa huduma kwa wananchi.

"Badala ya wananchi kwenda kufuata huduma za rufani Muhimbili, huduma hizo watazipata Mtwara," alisema.

Wenyeviti wa vijiji waliishukuru serikali kwa jitihada zake za kuboresha huduma mbalimbali za kijamii katika maeneo yao zikiwamo za afya, maji, elimu na miundombinu.

"Suala la afya tupo vizuri, tuna zahanati ya kisasa na kuhusu maji wanatapa maji safi na salama," alisema Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbecha, Twalib Nandonde.

# Vigogo CCM wazindua kampeni Mbarali

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimezindua kampeni zake katika Jimbo la Mbarali, huku mgombea anayewania jimbo hilo, Bahati Ndingo akiomba serikali kuruhusu wakulima waendelee kulima maeneo ambayo yanafanyiwa tathimini.

Akihutubia wananchi jana katika kampeni hizo eneo la Stendi ya Rujewa, aliwaomba wajumbe wa Kamati Kuu ya CCM waliokuwapo kufikisha kilio cha changamoto ya ardhi kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya ufumbuzi ili wananchi waruhusiwe kulima maeneo yaliyozuiliwa wakati taratibu zikiendelea.

"Tuna migogoro ya ardhi, tunaomba turuhusiwe kulima maeneo yasiyoruhusiwa kulima. Hawa wananchi asilimia kubwa ni wakulima, tunaomba turuhusiwe wakati mambo mengine yanashughulikiwa na serikali kuu," aliomba.

Wajumbe wa Kamati Kuu waliohudhuria uzinduzi huo ni Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini na Katibu wa Oganaizesheni, Issa Gavu.

Pinda akizungumza katika kampeni hizo alisema Kamati Kuu ya CCM ilipoketi kulikuwa na mapendekezo ya watu 25, lakini mgombea huyo ndiye aliyeongoza kuanzia ngazi ya awali na wana imani na uchapakazi wake huku akiwataka wananchi kutofanya makosa kwenye uchaguzi.

Dk. Tulia alisema Bahati ana ushirikiano mzuri na wenzake na ndio maana jana alikuwa Mbeya



Mjini.

"Ni mtu mwenye ushirikiano mzuri na wabunge wenzake, ndio maana wabunge wenzake tumejikusanya hapa, tunaamini Septemba 19, atakuwa mbunge ninamfahamu uhodari wake," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Tulia, tangu Bahati akiwa mbunge wa Viti maalumu amefanya kazi kubwa ya kuuliza kuhusu hoja za wananchi wa Mbarali na kuchangia michango mbalimbali.

"Nawaambia mnaye mtu sahihi atawakilisha vema mpeni kura awe mwakilishi wenu, msiwe na wasiwasi CCM ndio kina wajibu wa kushughulikia hoja zenu," alisema Dk. Tulia.

Gavu aliwataka wananchi wa Mbarali kutofanya makosa ya kumpa mtu mwingine nafasi ya ubunge, akisema nafasi hiyo ya uwakilishi huwa haijaribiwi.

Uchaguzi wa marudio unafanyika baada ya kifo cha Mtega aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo kilichotokea Julai mosi, mwaka huu kwa kugongwa na trekta.

Kabla ya kuwania nafasi hiyo, Bahati alikuwa mbunge wa viti maalumu Mkoa wa Mbeya, lakini alijiuzulu nafasi baada ya Kamati Kuu ya CCM kumteua kugombea jimbo hilo.


**KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LIMITED (KCJE LTD)**

## TANGAZO LA ZABUNI

**ZABUNI NA : KCJE/2023-2024/ZABUNI/03: USAMBAZAJI WA KUMPYUTA MPAKATO (LAPTOPS) 702.**

**11/09/2023**

1. ***"Korosho Cooperative Joint Entreprise Limited"*** ni Ushirika wa Mradi wa Pamoja chini ya Kifungu cha 33 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2015.
2. Kwa idhini ya "Korosho Cooperative Joint Entreprise Limited" Mwenyekiti, anatangaza Zabuni ya usambazaji wa kumpyuta mpakato (Laptops) 702.
3. Aidha, Kampuni zenye sifa, vigezo na uwezo wa kusambaza kumpyuta mpakato, zinaombwa kuwasilisha maombi yao kwa kuzingatia sifa mahsusi za mahitaji yaliyoanishwa hapo chini kama ifuatavyo

**SIFA ZA KOMPYUTA MPAKATO**

| Na | Features | Specifications |
|---|---|---|
| 1. | Operating System | **Genuine** Microsoft Windows 10 (64 Bit) |
| 2. | Processor | Inter ® Core i3 or Above 12 Generation and Above |
| 3. | Memory | RAM 4GB or above |
| 4. | Hard Disk Drivers | 500 GB or Above |
| 5. | Audio | Bang & Olufsen, dual speakers, Audio Boost with all installed drivers |
| 6. | Communications/Wireless Audio | Integrated Network Card Local Area Network (LAN): 10/100/1000MBPS Wireless Local Area Network (WLAN): 802.11 ac Wireless LAN or latest USB 3.0 Connectivity, HDMI Ports, 2 Slots or More Mobile Broadband Module (Recommended) |
| 7. | **I/O** Devices | Keyboard: Illuminated Backlit, Spill-resistant keyboard with drain Webcam: Yes |
| 8. | Supplemental Items | Stereo headphone/ Microphone Combo CD/DVD, R/RW Drive: Internal or External Leather Case Mouse |
| 9. | Display | 14" (35.5 cm) diagonal FHD IPS BrightView micro-edge WLED - backlit (1920 X 1080) |
| 10. | Software | Genuine Microsoft Office 365 |
| 11. | Minimum Warrant | 12 Months |

4. Nyaraka za zabuni zinapatikana kwa malipo ya shilingi mia tano elfu tu (500,000/=) malipo hayo yapitie kwenye:-

**AKAUNTI NAMBA: 0150771321300**
**JINA LA AKAUNTI: KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LTD**
**BENKI: CRDB – TAWI LA MTWARA**

5. Mwombaji awe na uzoefu usiopungua miaka mitatau (3).
6. Mchakato wa zabuni hii utafanyika kwa njia shindani ya Kitaifa (NCT) kwa mujibu wa Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 na marekebisho yake ya 2016 na ni zabuni ya wazi kwa wazabuni wote wenye sifa stahiki.
7. Wazabuni wote wanakaribishwa ofisi ya Katibu wa Mradi wa Pamoja (Korosho Cooperative Joint Enterprise Limited) iliyopo Wilaya ya Mtwara Mtaa wa MADUKA MAKUBWA Jengo la Ushirika wa TANECU LTD Ghorofa ya Kwanza kwa ajili ya kuwasilisha maombi muda wa saa za kazi kuanzia saa mbili asubuhi (8:00hrs) hadi saa kumi na nusu jioni (16.30hrs) isipokuwa siku za Jumamosi na Jumapili pamoja na siku za siku kuu.
8. Wazabuni wote wawasilishe zabuni zao katika Nakala tatu (nakala halisi moja, na nakala kivuli mbili) zikiwa zimefungwa kwa umakini na kuwekwa lakiri. Zabuni zote zitafunguliwa mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha. Tukio ambalo litakuwa la wazi kwa wazabuni na wawakilishi wa wazabuni watakaohudhuria.

Mwisho wa kupokea ni siku ya 02/10/2023 saa nne kamili asubuhi (10:00hrs) katika Ukumbi wa Mikutano wa TANECU LTD Mjini Mtwara. Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo: -

**Mwenyekiti,**
**Korosho Cooperative Joint Enterprise Limited,**
**S.L.P 660,**
**MTWARA**

9. Zabuni zote zitakazochelewa hazitafikiriwa wakati wa tathimini bila kujali sababu zozote za kuchelewa.
10. Zabuni zitakazotuma email, telegram au fax zabuni yake haitafunguliwa wala kufanyiwa kazi.

**IMETOLEWA NA**

**MWENYEKITI**
**KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LTD**
**S.L.P 660,**
**MTWARA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars imetuheshimisha, ikawe hivyo kwa Simba, Yanga CAF

**KONGOLE** nyingi kwa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kwa kufanya makubwa dhidi ya vigogo wa soka Afrika, Timu ya Taifa ya Algeria, baada ya kulazimisha suluhu ugenini, hivyo kukata tiketi ya kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast.

Katika mechi hiyo ya mwisho ya hatua ya makundi, Stars ilikuwa ikihitaji sare yoyote ama ushindi ili kuungana na Waalgeria hao ambao walishafuzu, kuwa timu mbili kutoka Kundi F, zitakazoshiriki michuano hiyo itakayoanza kutimua vumbi hapo Januari 13, mwakani.

Kama Stars ingepoteza ni wazi Uganda iliyopata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Niger, ndiyo ingefuzu kwani ingefikisha alama saba sawa na Tanzania, lakini ingekuwa na tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Hivyo, kwa ilichokifanya Stars kupata sare ugenini dhidi ya Algeria ikafikisha alama nane, hivyo ni jambo la kupongezwa kuanzia kwa wachezaji, benchi la ufundi, Shirikisho la Soka nchini (TFF), pamoja na serikali kwa ujumla chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa mstari wa mbele si tu katika kuhakikisha sekta ya michezo nchini inakuwa bali pia kwa kutoa motisha kuanzia kwa klabu hadi timu za taifa pale zinapofanya vizuri kwenye mechi za mashindano ya kimataifa.

Kinachopaswa kufanywa na Stars kwa sasa, ni TFF, serikali pamoja na wadau wote wenye mapenzi mema na soka la nchi hii, kuhakikisha maandalizi mema yanaendelea kufanyika kuelekea fainali hizo ili timu hiyo ikifika Ivory Coast hapo mwakani iwe mshindani wa kweli na si kuishia kushiriki tu.

Tunaamini kama Stars imeweza dhidi ya Algeria ugenini, maandalizi yakifanyika vema hata Ivory Coast itaenda kuwashangaza wengi kwani uwezo huo upo na wachezaji wanaweza kama wakiwezeshwa ipasavyo.

Baada ya pongezi hizo, kwa wachezaji wa Klabu za Simba, Yanga na Singida Foutain Gate FC na wale wa kimataifa waozichezea, ambao waliokuwa kwenye majukumu yao na timu zao za taifa, hawana budi sasa kusahau matokeo hayo, kwa wale ambao timu zao zimefuzu na hata waliopoteza, ni wakati wa kugeukia michuano mingine ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Ligi ya Mabingwa na Shirikisho Afrika.

Wote tunatambua Jumamosi wiki, wakongwe wa soka nchini, Simba na Yanga watashuka katika viwanja tofauti ugenini kucheza mechi za raundi ya kwanza za Ligi ya Mabingwa Afrika kungali Ijumaa Singida Fountain Gate ikiwa nyumbani kuikaribisha Future FC ya Misri kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba itashuka katika Uwanja wa Levy Mwanawasa nchini Zambia kuvaana na Power Dynamos saa 10 alasiri wakati huo Yanga yenyewe ikivaana na Al-Merrikh kwenye Uwanja wa Pele nchini Rwanda majira ya saa moja usiku.

Kwa upande wa Singida Fountain Gate yenyewe Ijumaa itashuka katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam kuikaribisha Future FC kwenye mechi ya kwanza ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Al Merrikh inautumia Uwanja wa Pele, Rwanda kama wake wa nyumbani kutokana na hali ya machafuko ya kisiasa yanayoendea nchini kwao, Sudan. Miamba hiyo itarudiana Oktoba 29, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na timu itakayopata matokeo ya jumla, itatinga hatua ya makundi, kadhalika kwa Singida Fountain Gate FC itakayokwenda kumalizia ugenini.


Kwa mantiki hiyo, wawakilishi hao wa nchi kwenye michuano hiyo ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, hususan ni Simba na Yanga, wanapaswa kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ugenini, ili kurahisisha kazi na kutocheza kwa presha kwenye mechi za marudiano nchini lakini pia kwa Singida kutofanya makosa ikiwa nyumbani.

Tunataka kuona furaha iliyotupa Stars kwa kufuzu AFCON 2023, Simba, Yanga na Singida FC zinakwenda kuiendeleza kwa kufuzu hatua ya makundi kwa kuanza kupata ushindi wa kishindo katika michezo yao hiyo ya kwanza na kisha kufuzu hatua ya makundi, robo fainali, nusu na fainali kabisa.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Karia naye apewe maua yake Taifa Stars kufuzu AFCON 2023

Na Adam Fungamwango

**HAITOKUWA** vema hata kidogo kuipongeza Taifa Stars kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), bila kumtaja Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Wallace Karia.

Ukiangalia sana unaweza kusema ana bahati kubwa tangu aingie madarakani. Halafu ukifikiria tena zaidi utakuta pia kuna kazi kubwa ambayo anaifanya ambayo imesababisha yote haya.

Ni wakati wa uongozi wake ndiyo tunaona vitu ambavyo huko nyuma ilikuwa ni ndoto kwa Watanzania. Tanzania ilisubiri kufuzu AFCON kwa miaka 39, tangu ilipofanya hivyo mwaka 1979, ila tangu aingie madarakani tayari Stars imefuzu mara mbili chini yake.

Ni miaka mitatu tu imepita tangu Tanzania ilipofuzu 2019, na sasa 2023 imefuzu tena kwenda katika fainali hizo zitakazochezwa mwakani nchini Ivory Coast kuanzia Januari 13 hadi Februari 11.

Wengi wanaangalia juu juu kuwa Stars imefuzu, lakini wanashindwa kujua mpaka nchi ifuzu kuna mambo mengi ambayo yanatakiwa yafanywe sawasawa na viongozi wa shirikisho kama vile kuwa na ligi bora, maandalizi, mipango, usafiri, malazi, posho na mengine yanayofanana na hayo ikiwamo benchi bora la ufundi.

Ukitaka kuona haya yote hayatokei kwa bahati mbaya, ni kwamba kipindi cha Karia ukiachilia mbali Stars kufuzu mara mbili kwa kipindi kifupi, ndicho kipindi ambacho Klabu ya Simba imefuzu mara tano hatua za makundi mechi za kimataifa, mara nne Ligi ya Mabingwa Afrika na mara moja Kombe la Shirikisho. Na ndicho kipindi ambacho Klabu ya Yanga imefika fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Klabu za taifa za soka wanawake kwa umri mbalimbali zimetwaa mataji na kupata mafanikio makubwa, tukiwa pia na kumbukumbu ya timu ya soka ya Taifa ya Wanawake walio chini ya miaka 17 'Serengeti Girls' kufuzu kwa mara ya kwanza Kombe la Dunia na fainali zake kuchewa nchini India.

**Ni miaka mitatu tu imepita tangu Tanzania ilipofuzu 2019, na sasa 2023 imefuzu tena kwenda katika fainali hizo zitakazochezwa mwakani nchini Ivory Coast kuanzia Januari 13 hadi Februari 11.**

Kama vile haitoshi, Klabu za Simba Queens na JKT Queens kutwaa ubingwa wa CECAFA. Kwa mara ya kwanza Simba Queens ilikwenda kuiwakilisha nchi na Ukanda wa Afrika Mashariki kwa ujumla kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake na tayari JKT Queens imeshakata tiketi hiyo.

Hakika haijawahi kutokea kiongozi yoyote wa soka nchini akapata mafanikio yote haya wakati wa utawala wake kama Karia. Ameruhusu wachezaji wengi wa kigeni kumiminika nchini ambao mbali na kuzifanya klabu kuwa bora, lakini wamewafanya wachezaji wetu kujiongeza na inafika sehemu hawana tena hofu wanapocheza na timu kutoka nje ya nchi, wala kuhofu wanapocheza ugenini.

Ni kwa sababu tayari wameshazoea wanapocheza kwenye klabu zao michuano ya kimtaifa ambako wanafanya vizuri. Kumekuwa na tabia ya baadhi ya watu na wadau wa soka ikitokea changamoto ndogo tu, lawama inakuwa kwa Karia. Refa kachezesha vibaya lawama kwake, timu imefungwa kimpira, lakini anaambiwa yeye kuwa ndiye kasababisha.

Mapungufu ya watu wengine wachache au ya kimfumo, yasimfanye atupiwe lawama, bali tukumbuke nyuma soka letu lilipotoka. Nina uhakika kuwa kwa sababu hizi sasa mafanikio yanaonekana, lakini huko mbele tutakapoyakosa na kuyasaka tena, tutamuandika kwa wino wa dhahabu kiongozi huyu.

Tunatakiwa naye tumpongeze kwa yote aliyoyafanya, na hata kwa hili la Stars kutinga tena AFCON tusije kumuacha nyuma, anatakiwa apewe maua yake kwa uongozi thabiti, usioyumba ambao ndiyo umeleta mafanikio yote haya.

## Samia, Majaliwa wawasisitiza matumizi stakabadhi ghalani

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imesisitiza dhamira yake ya kuendelea kuwaunganisha wakulima nchini na masoko ya mazao yao huku ikitoa wito kwa wakulima wa mazao mbalimbali kuendelea kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani katika mauzo ya mazao yao.

Hilo linatokana na mafanikio makubwa yanayotokana na mfumo huo hususani katika kuchochea ongezeko la bei ya mazao.

Wakizungumza kwa nyakati na matukio tofauti hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, walisema kwa sasa bei za mazao ya korosho, mbaazi, kakao na ufuta zimeongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na ushindani uliopo miongoni mwa wanunuzi wa mazao hayo unaochochewa na mfumo wa stakabadhi ghalani.

"Ni kweli kwamba kwa sasa muunganiko kati ya mkulima na masoko bado hauridhishi. Hata hivyo, jitihada ambazo tumeanza kuzifanya kwenye baadhi ya mazao ikiwamo korosho na mbaazi zimesaidia kupandisha bei ya mazao hayo.

"Kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani tumefanikiwa kuwaunganisha wakulima na wanunuzi moja kwa moja bila kuwapo watu wa kati (dalali) ambao hapo awali walikuwa wananunua mazao yakiwa shambani kwa bei ya chini zaidi," alisema Rais Samia aliposhiriki majadiliano katika Jukwaa la Mifumo ya Chakula (AGRF) lililohitimishwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Katika kuthibitisha umuhimu wa mfumo wa stakabadhi ghalani, Rais Samia alitoa mfano wa zao la mbaazi ambalo msimu wa kilimo uliopita liliuzwa Sh. 00 kwa kilo, lakini kwa msimu huu limeuzwa kwa bei ya Sh. 2,000 na zaidi.

"Na huo (mfumo wa stakabadhi ghalani) ndio mtindo ambao tutakwenda nao kwenye mazao mengine pia," alisisitiza Rais Samia huku akiahidi kuongeza zaidi kasi ya ujenzi wa barabara za wilaya mbalimbali nchini ili kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka kwa wakulima kwenda kwenye masoko ya mazao yao ndani na nje ya nchi.

Akizungumza wakati akihairisha shughuli za Bunge mwishoni mwa wiki, Waziri Mkuu Majaliwa alisema kwa sasa bei za mazao nchini zinaendelea kuimarika zaidi huku akibainisha kuwa hali ni nzuri zaidi kwa mazao yanayouzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

"Mathalani, zao la kakao linalolimwa kwa wingi katika wilaya za Kyela na Mvomero limeuzwa kwa Sh. 8,700 kwa kilo kutoka bei ya Sh. 2,500 kwa kilo hapo awali.

"Kwa upande wa zao la ufuta, lenyewe limeuzwa kwa Sh. 4,000 kwa kilo kutoka bei ya Sh. 1,000 hadi 1,200 kwa kilo msimu uliopita," Majaliwa alisisitiza.

**"Mathalani, zao la kakao linalolimwa kwa wingi katika wilaya za Kyela na Mvomero limeuzwa kwa Sh. 8,700 kwa kilo kutoka bei ya Sh. 2,500 kwa kilo hapo awali.**



Rotary Gavana wa Wilaya ya 9214 , Francisco Semwanga akimkabidhi mzazi mtarajiwa msaada wa vifaa vya kujifungua wakati wa hafla ya kutoa msaada wa vifaa hivyo kwa wazazi tarajiwa iliyofanyika katika hospitali ya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ajira 100,000 zaja kongani ya viwanda

**Na Joseph Mwendapole**

KONGANI ya Viwanda ya Sino Tan Industrial Park iliyoko Kwala wilayani Kibaha, mkoani Pwani, inayotarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 320, itatengeneza ajira 100,000 za moja kwa moja.

Vilevile, kongani hiyo ambayo itakuwa na viwanda 200, itatengeneza ajira zisizo za moja kwa moja 500,000 kwa wazawa ambao watafanya kazi katika viwanda hivyo.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Sino Tan, Janson Huang, alipozungumza na ujumbe wa Shirikisho la Viwanda (CTI), uliotembelea eneo hilo kuangalia maendeleo yake.

Huang alisema ujenzi wa eneo hilo ulianza Mei mwaka jana baada ya kukabidhiwa eneo hilo na serikali. Wanatarajia kukamilisha ujenzi huo ndani ya miaka mitano ijayo.

"Mwaka mmoja uliopita eneo hili lilikuwa pori kubwa na hakukuwa na barabara kutoka njia kuu ya Morogoro kuja hapa, lakini kwa mwaka mmoja tu tumeweza kujenga barabara ya lami kuja hapa na majengo makubwa. Kwahiyo, tunatarajia ndani ya miaka mitano patakuwa sehemu ya kuvutia," alisema.

Vilevile, alisema wamekuwa wakitangaza eneo hilo China na mataifa jirani na wawekezaji wengi wameonesha nia ya kuja kuwekeza. Mwezi huu wanatarajia kuanza kupokea viwanda vinne kuwekeza eneo hilo.

Alisema mwakani wanatarajia kupokea viwanda kati ya 15 na 20. Nia ya Sino Tan ni kujenga kongani ya viwanda ambayo kwa mwaka itakuwa na uwezo wa kuzalisha Dola za Marekani bilioni sita.

Alisema wameshazungumza na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wakitaka kuanzisha chuo cha mafunzo ya ufundi eneo hilo ili kufundisha wataalamu watakaofanya kazi katika viwanda vya eneo hilo.

"Tunataka kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda kwa kurithisha teknolojia kwa Watanzania watakaofanya kazi viwandani, ndiyo maana tunataka kujenga chuo cha ufundi kufundisha vijana wa Kitanzania hapahapa," alisema.

Alishukuru CTI kwa kuwatembelea mara kwa mara kuangalia maendeleo ya ujenzi na aliahidi wataendelea kutoa ushirikiano kwao kwa kuwa wamekuwa wakiwasaidia kutangaza eneo hilo.

Mkurugenzi wa CTI, Leodegar Tenga, alipongeza Kampuni ya Sino Tan kwa uamuzi wake wa kujenga kongani hiyo. Itasaidia kuvutia wawekezaji kutokana na kuwa na eneo kubwa.

"Hili ni eneo la kimkakati kwa sababu mwekezaji akija hapa anakuja na mashine zake tu. Anakuta kila kitu kiko hapa, anakuja majengo yapo, ofisi zipo, maji, umeme upo. Ninawapongeza sana kwa sababu eneo hili litachangia sana kuinua uchumi," alisema. Tenga pia aliwataka wawekezaji wenye viwanda ndani na nje ya nchi kuchangamkia fursa hiyo kwa kuwa kuwekeza katika eneo hilo kutawapunguzia gharama ya kufanya maandalizi ya uzalishaji.

Samuel Nyantahe, Mwenyekiti mstaafu wa CTI, alisema Sino Tan wamejipanga vizuri kwa kuwekeza katika eneo la ekari 2,500 ambalo litawarahisishia wawekezaji. Badala ya kuanza ujenzi wa miundombinu, wanaanza uzalishaji mara moja.

Mwanachama wa CTI, Evarist Maembe, alifurahishwa na kasi ya maendeleo ya ujenzi wa kongani hiyo ambayo itakuwa ya aina yake kwa Afrika Mashariki kutokana na ukubwa wake.

"Kwa kasi hii ninaona kabisa ile dhana ya Tanzania ya viwanda inakwenda kutimia kwa sababu kutakuwa na miundombinu yote ya kuwezesha mwekezaji kufanya shughuli zake kwa urahisi kwa sababu hata taasisi za serikali zitakuwa na ofisi zake hapa," alisema Maembe.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Dk. Mwinyi apongeza CRDB kwa huduma kuzingatia imani ya dini

**Na Mwandishi Wetu,**
UNGUJA

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Benki ya CRDB kwa kuanzisha huduma za kibenki zinazofuata misingi ya sharia, hivyo kuwahamasisha Waislamu wengi kutumia huduma zake na kuchochea ujumuishi wa kifedha.

Dk. Mwinyi ambaye alikuwa mteja wa kwanza kufungua akaunti ya Al Barakah mwishoni mwa mwaka 2021 huduma hiyo ilipozinduliwa, alitoa pongezi hizo alipokabidhiwa kadi ya akaunti hiyo mwishoni mwa wiki alipotembelewa na ujumbe wa Benki ya CRDB Ikulu, mjini Zanzibar.

"Tulijua Al Barakah itakuwa na mafanikio, lakini hatukutarajia kuwa yangepatikana ndani ya muda mfupi namna hii.

"Ninawapongeza kwa mafanikio mliyoyapata na niwaahidi kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendeleza ushirikiano na benki yenu kuhakikisha huduma hizi zinawafikia Waislamu wengi walipo visiwani humu ili kwa pamoja tushiriki kulijenga Taifa letu huku tukimwabudu Mwenyezi Mungu bila kukiuka maagizo yake," alisema.

Rais Dk. Mwinyi pia alishukuru Benki ya CRDB kwa heshima iliyompa ya kuwa mteja wa kwanza kukabidhiwa kadi ya Akaunti ya Al Barakah na akasema jambo hilo limemhamasisha zaidi, hivyo ataangalia namna ya kuongeza amana kwenye akaunti yake ili kufurahia huduma hizo zinazokidhi mahitaji yake ya kifedha na imani ya kiroho.

Akimkabidhi kadi ya Al Barakah, Meneja wa Kanda ya Mashariki wa Benki ya CRDB inayojumuisha Zanzibar na mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, Badru Idd, alisema Rais Mwinyi si tu alihamasisha kuanzishwa huduma hizo, bali pia alionyesha mfano kwa kuwa wa kwanza kufungua akaunti hiyo mwaka 2021 ambayo mpaka sasa ina wateja zaidi ya 70,000 nchini kote.

"Mpaka sasa hivi, tumekopesha zaidi ya Sh. bilioni 90 kwa misingi ya sharia na tumepokea amana za wateja zaidi ya Sh. bilioni 85 ndani ya miaka miwili ya kutoa huduma hizi.

"Huduma za CRDB Al Barakah Banking zinaendelea kutoa mchango mkubwa sana katika serikali yako ya Zanzibar na wananchi wake kwa kuwa tumekopesha zaidi ya Sh. bilioni 18 kwenye uchumi wa bluu na wafanyabiashara wamepata zaidi ya Sh. bilioni 33," alisema Idd.

Ili kusogeza huduma kwa wananchi visiwani hapa, Benki ya CRDB ilifungua tawi mjini Wete lililozinduliwa na Rais Dk. Mwinyi mwaka 2021 alikoomba benki kuanzisha huduma zenye misingi ya sharia na mpaka sasa kwenye matawi manne ya Benki ya CRDB yaliyomo Zanzibar, wananchi wameweka amana za zaidi ya Sh. bilioni 28.

Kuhusu kadi za Akaunti ya Al Barakah, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Benki Zinazofuata Sharia (Islamic Bankink) wa Benki ya CRDB, Rashid Rashid, alisema kadi hizo za aina nne na zote zinaweza kutumika katika majukwaa yote ikiwamo kwa mawakala zaidi ya 200 walipo Zanzibar kama ilivyo kwa kadi zinazotumiwa na wateja wengine wote wa Benki ya CRDB.

"Pamoja na mafanikio haya makubwa, CRDB Al Barakah Banking tunaendelea kuboresha huduma zetu ili kuwafikia wateja wetu na kuwapa amani wanayoitegemea kwa kuweka fedha zao katika akaunti za Al Barakah zinazofuatisha misingi ya sharia.

"Kila mteja mwenye akaunti hii, ana amani kwa kujua kwamba fedha zake ziko mahala salama na zina uangalizi maalum unaoendana na imani na maadili yake," alisema Rashid.

Akizungumzia umuhimu wa huduma za fedha kwa maendeleo ya Taifa, Mwenyekiti wa Bodi ya Huduma za Fedha Zinazofuata Misingi ya Sharia ya Benki ya CRDB, Abdul van Mohammed, alisema kuna fursa nyingi ambazo Zanzibar inaweza kunufaika nazo iwapo itafungua milango.

"Zanzibar ndiyo yenye matumizi makubwa ya Islamic Banking Afrika Mashariki. Ninaomba serikali iangalie uwezekano wa kuifanya kuwa ya kwanza kuuza hatifungani ya Kiislamu ili kupata fedha zitakazochangia maendeleo ya watu wetu," alisema Mohammed.




Meneja wa Kanda ya Mashariki wa Benki ya CRDB, Badru Idd akimkabidhi Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi mfano wa kadi ya akaunti ya Al Barakah inayoendeshwa kwa misingi ya sharia katika hafla iliyofanyika Ikulu ya Zanzibar mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## Waziri Silaa: Tujenge nidhamu ya wizara

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amewataka watumishi wa wizara yake kuhakikisha wanatoa huduma vizuri kwa wananchi ili wajenge imani na serikali.

"Lazima tutengeneze nidhamu ya wizara kwa kuwahudumia vizuri wananchi. Tukumbuke hapa tunafanya kazi ya Watanzania kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Waziri Silaa alipozungumza na watumishi wa Wizara ya Ardhi mwishoni mwa wiki.

Ni baada ya uzinduzi wa Kituo cha Taifa cha Ubunifu na Mafunzo ya Taarifa za Kijiografia. Alisema kuwa wakati wa kutekeleza majukumu, watumishi hao wakumbuke kuwa si kila mwananchi ana haki, lakini wanao wajibu wa kutenda haki wakati wote wa utekelezaji majukumu.

"Mna wajibu wa kusimamia haki na kila mtu atolee uamuzi kwa kazi inayowasilishwa kwake na kama mwananchi hapaswi kupewa kiwanja, aelezwe bayana kwa maandishi," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri wa Ardhi, wizara hiyo kwa sasa inakwenda kufanya maboresho yanayolenga kuleta tija. Watumishi wa sekta ya ardhi wawe tayari kwa maboresho hayo.

"Mtu anafuatilia hati kwa zaidi ya miezi mitatu. Hapo pana alama ya kuuliza. Hata kama ni urasimu utakuwa umepitiliza," alionya.

Waziri huyo aliwaeleza watumishi wa wizara hiyo kuwa pamoja na kuelezwa mambo mengi ya wizara yake, ana haki ya kusikiliza na kubainisha atazitumia siku 100 kujifunza ili watakapokutana kwenye maeneo ya kazi ajue cha kufanya.

Kikao hicho cha Waziri Silaa na watumishi kimehusisha viongozi wa wizara, baadhi ya watumishi kutoka Makao Makuu, Ofisi za Ardhi za Mikoa na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

# Kampuni ya saruji kumlipa mkurugenzi wake mabilioni

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam imewaamuru ndugu na wakurugenzi wawili wa Kampuni ya Saruji Dar es Salaam kumlipa Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu wao, Pardeep Hans, zaidi ya Sh. bilioni 10 kwa kumfukuza katika kampuni hiyo na kuiuza kwa kampuni nyingine.

Jaji Amir Mruma alifikia uamuzi huo baada ya kukubali shauri lililofunguliwa na Wakili Joseph Rutabingwa kwa niaba ya Pardeep ambaye alikuwa Mwanahisa Mkuu wa kampuni hiyo, dhidi ya ndugu hao wawili ambao ni Merey Saleh na Ismail Saleh.

Alibainisha kuwa uuzaji na uhamishaji wa mali za kampuni hiyo katika eneo la Mbagala kwenda Kampuni ya Amsons Industries uliofanywa na ndugu hao wawili ulikuwa batili.

Jaji Mruma alisema ushahidi uliotolewa ulithibitisha madai ya mauzo hayakufuata utaratibu na sheria. Yalifanywa na wanahisa wadogo bila kumshirikisha Mwenyekiti, Mkurugenzi Mkuu na Mwanahisa Mkuu wa Kampuni.

"Vitendo hivi vilifanyika bila kumshirikisha mlalamikaji ambaye ndiye Mkurugenzi Mkuu na Mwanahisa Mkuu wa Kampuni ya Saruji ya Dar es Salaam," alisema Jaji Mruma.

Vilevile, aliamuru ndugu hao wawili kumlipa mlalamikaji Sh. milioni 72.5 ikiwa ni kiasi kilicholipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ( TRA) kama kodi ya uhamisho wa hisa kwake.

Pia aliamuru kila mmoja wa ndugu hao amlipe mdai Sh. bilioni moja kiasi ambacho walilipwa kwa ajili ya ununuzi wa hisa hizo.

Pia, aliwaagiza ndugu hao kumlipa mdai Sh. bilioni 5.25 kama sehemu ya bei ya ununuzi wa hisa ambayo ingepatikana kutokana na gawio.

Jaji pia aliwaagiza kulipa Sh. bilioni 3.07 kama marejesho ya fedha zilizolipwa Benki ya Exim katika kutekeleza mkopo uliotolewa kwa manufaa ya kampuni hiyo ya saruji.

Jaji Mruma pia aliamuru walalamikiwa kulipa riba kwa kiwango cha asilimia 15 kwa mwaka kutoka siku ya kufungua shauri hadi siku ya hukumu na riba nyingine ya kiwango cha asilimia tatu kutoka siku ya hukumu hadi ulipaji kwa ujumla utakapofanyika.

Kabla ya kutoa nafuu hizo, Jaji Mruma alilazimika kuamua baadhi ya hoja zilizojengwa katika shauri hilo, ikiwamo iwapo makubaliano ya kuuza na kuhamisha sehemu ya hisa walizokuwa nazo ndugu hao wawili kwa mlalamikaji yalikuwa na masharti yoyote ya awali na iwapo yalitimizwa.

Pia, alizingatia kama mkopo uliotolewa na Benki ya Exim na kudhaminiwa na mlalamikaji ulitumika kwa manufaa ya Kampuni ya Saruji ya Dar es Salaam na kwamba uamuzi uliotolewa na kampuni hiyo bila kuwapo kwa mlalamikaji ulikuwa halali.

Katika hukumu yake aliyoitoa jijini Dar es Salaam, Jaji Mruma alipitia ushahidi uliotolewa na pande zote na kubaini makubaliano ya kuuza na kuhamisha sehemu ya hisa yaliwekwa katika baadhi ya masharti na si masharti ya awali kama walalamikiwa wangependa mahakama kuamini hivyo.

Jaji Mruma alisema kuwa ripoti ya upekuzi kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inaonesha kuwa taarifa za Kampuni ya Saruji ni kwamba ndugu hao wawili walikuwa na hisa 5,000 kila mmoja huku mlalamikaji akiwa na hisa 10,000.

Hivyo, alisema uamuzi wa kuiuza kampuni hiyo bila kumshirikisha yeye kama mwanahisa mkuu, hauwezi kuwa halali.



## TMSA kufungua kongomano la masoko 2023

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

CHAMA cha Wataalamu wa Masoko Tanzania (TMSA), kinatarajiwa kufungua kongamano la masoko kwa mara ya nne na kutoa tuzo za masoko kwa mara ya tatu mfululizo katika vipengele 20 tofauti mwaka huu, kuhamasisha weledi zaidi kwenye sekta ya masoko.

Tuzo hizo za masoko 2023, zitafanyika Oktoba 27 mwaka huu Jijini Dar es Salaam. Tangu mwaka wa 2021, TMSA imetumia tuzo hizo ili kuakisi juhudi na mafanikio ya watu binafsi, mashirika, na wasomi ambao wanaleta mabadiliko katika nyanja ya masoko.

Akizungumza jana kuhusu tuzo hizo, Mkurugenzi wa TMSA, Dk. Emmanuel Chao (PhD), alisema utaratibu huo unalenga zaidi kuonyesha ni jinsi gani masoko ni nguzo muhimu ya ukuaji wa kampuni na kuleta faida.

"Katika biashara yoyote, idara ya masoko ni ya kipekee, kwani inajumuisha kati ya asilimia 30 na 40 ya bajeti ya biashara, na ndio kati ya msingi wa kudumisha biashara yoyote.

"Kwa hiyo kama TMSA, tutatumia fursa hii kuhimiza kampuni na watendaji kuwa na weledi zaidi katika hii idara. Na kwa bahati nzuri, katika TMSA, tayari tunatoa programu za masoko. Pia tuko kwenye mazungumzo na Taasisi ya Chartered Marketing Institute ya nchini Uingereza.

...Nia yetu ni kuhakikisha soko la ndani linafaidika zaidi kwa kuzalisha wataalamu waliohitimu na wenye uelewa zaidi wa soko la Afrika kuliko soko la nje."

Mmoja wa wadhamini wakuu wa kongamano na tuzo hizo kutoka Kampuni ya Smart Codes, Iche Omari, alisema kuwa tuzo hizo zitakuwa chachu katika kuchochea ukuaji wa sekta ya masoko.

"Tuko pamoja na TMSA katika utoaji wa tuzo hizo, na matumaini yetu ni kuwa huu ni mwelekeo sahihi wa kuhamasisha ubunifu na weledi miongoni mwa wafanyabiashara wa Tanzania," alisema.

Mchakato wa kuchagua na kuteua washindi wa tuzo uliendeshwa mtandaoni kupitia tovuti ya www.tma.tmsa.or.tz/nomination, watu binafsi na mashirika yaliteuliwa. Baada ya mchakato wa uteuzi huo, timu ya majaji wenye uzoefu ilipitia uteuzi uliopendekezwa na washindi waliochaguliwa.

# Mkurugenzi wa zamani H'shauri Siha na wenzake wanne waachiwa huru

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKURUGENZI wa zamani wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Rashid Kitambulio na wenzake wanne, waliokuwa wakikabiliwa na mashtaka 34 ya uhujumu uchumi, ikiwamo kumdanganya mwajiri wakati wa uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2015, wameachiwa huru.

Uamuzi wa kuwaachia huru washtakiwa hao, ulitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Moshi, Herieth Mhenga, aliyekuwa akisikiliza shauri hilo, la mwaka 2021.

Washtakiwa wengine waliokuwa wakikabiliwa na kesi hiyo ni watumishi watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Stanley Koola, Godson Lema na Samwel Mseselo. Yumo pia, mfanyabiashara wa vipuri vya magari katika mji mdogo wa Sanya Juu, Fredrick Kitaly.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Herieth alisema, Jamhuri imeshindwa kuthibitisha makosa yote 34 kutokana na kasoro zilizojitokeza wakati mashahidi wake wakitoa ushahidi wao.

"Nimeupitia ushahidi wa Jamhuri pamoja na vielelezo vilivyotolewa na upande wa utetezi, vikiwamo vibali vya ruhusa na barua za mialiko zilizotolewa kabla ya safari hiyo zikielekeza ni nini kifanyike, wakati watakapo kwenda Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwenye tarehe husika.

"Lakini pia barua iliyokuwa inatoa maelekezo ya nini kifanyike baada ya safari hiyo, maelekezo yaliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, nimeona upande wa Jamhuri umeshindwa kuthitisha shitaka hili dhidi ya watuhumiwa wote.

...Kwani kwa kupitia ushahidi wa shahidi wa 25, dereva ambaye alikuwa anaendesha gari lenye usajili namba STK 4990, ambaye anadai hakuwahi kwenda kwenye safari hiyo, wakati akihojiwa na wakili wa utetezi alikubali kwenda Dar es Salaam mara moja kwa siku saba, lakini hakueleza ni wakati gani alikwenda safari hiyo tofauti na inayoainishwa.

"Jamhuri hawakuweza kumleta mtu yeyote kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuthibitisha ya kwamba washtakiwa hawakwenda kwenye safari hiyo."

Alisema dosari mbalimbali zilizofanya Jamhuri kushindwa kuthibitisha makosa hayo ni pamoja na mgongano wa mashahidi, wakati walipokuwa wakiulizwa maswali ya madodoso na wakili wa utetezi katika kesi hiyo, Elia Kiwia.

Mahakama hiyo imewaona washtakiwa wote watano, hawana hatia katika makosa yote waliyoshtakiwa na inaamua kuwaachia huru.

Miongoni mwa mashtaka yaliyokuwa yakiwakabili ni kutengeneza nyaraka bandia, kwa lengo la kumdanganya mwajiri, kutumia vibaya madaraka, kula njama, kusaidia kutenda makosa, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na makosa ya kugushi nyaraka mbalimbali ili kujipatia fedha.

Katika kesi hiyo, Jamhuri ilikuwa na mshahidi 29, huku upande wa utetezi wakijitetea wenyewe, wakiongozwa na wakili wao.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili Suzan Kimaro kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Katika hati ya mashtaka, ilidaiwa kuwa katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2015, washtakiwa hao walifanya ubadhirifu wa fedha za umma na kuzitumia kwa manufaa yao.

Ilidaiwa, mshtakiwa wa kwanza, Stanley Koola, alidanganya kwamba alitengeneza magari matano kwa mshtakiwa wa tano, Fredrick Kitaly, huku akijua hakufanya hivyo.

Aidha, alidaiwa alidanganya alikodi ukumbi wa Angaza Women Centre kwa ajili ya shughuli za uchaguzi huo na vilevile alidanganya kwamba alilipia chakula kwa mmliki wa mgahawa Embassy Tea Room, kwa kulipia huduma Sh. milioni 12, huku akijua ni uongo.

Pia, anadaiwa alidanganya alikodi magari 53 katika shughuli hiyo ya uchaguzi, huku magari manane yakionekana kwa kipindi hicho yalikuwa bado hayajasajiliwa katika mfumo wa usajili wa magari wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hivyo kujipatia kwa udanganyifu Sh. milioni 34.

Makosa mengine ni mshtakiwa wa kwanza Stanley Koola, mshtakiwa wa pili, Rashid Kitambulio na mshtakiwa wa tatu, Godson Lema, kudaiwa walidanganya walikwenda Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuanzia tarehe 14/10/2015 hadi 21/10/2015 na kujipatia Sh. 980,000 kila mmoja kama pesa ya posho ya kujikimu, huku wakijua haikuwa kweli.

Kadhalika, kulikuwa na makosa mengine ya mshtakiwa wa kwanza, kudaiwa kudanganya kulikuwa na baadhi ya matumizi ya mafuta ya magari yaliyotolewa na vituo mbalimbali vya mafuta, yakiwemo mafuta yaliyodaiwa kutumika katika safari hiyo ya kwenda Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jijini Dar es salaam kwa ajili ya shughuli za uchaguzi.

Pia, Stanley Koola na Fredrick Kitaly walidaiwa kufanya ubadhirifu wa takribani Sh. milioni 32 huku Koola pamoja na Mseselo walituhumiwa kufanya ubadhirifu wa Sh. milioni 34.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kushoto) na Meneja Masoko wa Oryx Gas Kanda ya Mashariki Shaban Fundi (kulia) wakiwa wameshika mtungi wa gesi wenye ujazo wa kilo 15 kabla ya kukabidhi kwa mmoja ya wanawake wajasiriamali katika Jiji la Tanga mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 1.4/- zatolewa kusimamia uendelezaji miradi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya usimamizi na uendelezaji wa miradi mitatu mikubwa inayoendelea kutekelezwa katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya sekta ya elimu katika eneo hilo.

Serikali kuu imetoa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo, kupitia mradi wa uboreshaji wa miundombinu kwa shule za sekondari (SEQUIP).

Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu katika Halmashauri ya Arusha, Anna Urio, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akikagua miradi hiyo inayoendelea kujengwa kwa fedha zilizotolewa na serikali.

Aliitaja kuwa ni pamoja na ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Kata ya Moivo utakaogarimu Sh. milioni 587.4 hadi kukamilika.

Mradi mwingine ni ujenzi wa mabweni na ukarabati shule ya Sekondari Mringa kwa gharama ya Sh. milioni 360 na ujenzi wa nyumba ya walimu yenye sehemu mbili kwenye Shule ya Sekondari ya Kiutu kwa Sh. milioni 90.

Aidha, alisema kukamilika kwa miradi hiyo, kutatimiza adhma ya serikali ya kuwa na miundombinu bora kwenye shule kwa kuwa na mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia kwa walimu na wanafunzi, kadhalika kupunguza adha kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shuleni.

"Kwa niaba ya halmashauri yetu tunaishukuru serikali kwa kutoa fedha hizi kwa kuwa zitakwenda kuwa msaada mkubwa kwa shule zetu za sekondari kuwa na mazingira rafiki ya kujifunzia kwa wanafunzi na kufundishia kwa walimu," alisema.

Alisema mradi wa shule mpya ya sekondari Kata ya Moivo, utajumuisha ujenzi wa jengo la utawala, vyumba vinane vya madarasa, maabara tatu za sayansi na chumba cha TEHAMA.

Pia, ujenzi huo, utahusisha maktaba, matundu ya vyoo vya wasichana na wavulana, chumba maalum cha wanafunzi wenye ulemavu, kichomea taka kimoja na mnara wa tangi la maji lenye ujazo wa lita zaidi ya 20,000.

Alisema hadi sasa mradi huo, umefikia hatua ya kumwaga jamvi kwenye majengo yote sita na utagharimu Sh. milioni 584.





# Jamii yakumbushwa kulinda watoto dhidi ya ukatili

**Na Restuta Damian,** KAGERA

JAMII imekumbushwa kushiriki kikamilifu katika kulea na kulinda watoto dhidi ya ukatili unaotokea mara kwa mara na kusababisha kuongezeka mitaani na kukosa haki zao za kimsingi na kuishia kuwa wezi na tabia nyingine hatarishi.

Kauli hiyo imetolewa kwa nyakati tofauti na baadhi ya wakazi mkoani Kagera wakati wakihojiwa na Nipashe kuhusu namna sahihi ya kudhibiti vitendo vya ukatili kwa watoto ili waweze kuwa na misingi bora katika maisha.

Mkazi wa Kata ya Bukoba, Debora Julius, alisema jamii, wazazi na walezi wana wajibu wa kuwa na uangalizi wa malezi kwa watoto kuhusu matukio hayo ambayo yanaendelea kutendwa na wanajamii na kusahau kuwa wanawajibu pia wa kuwa walinzi wa kwanza wa watoto hao.

Alisema vitendo vya ubakaji, ulawiti na manyanyaso vimekuwa ni kasumba na kupoteza uelekeo wa makuzi ya mtoto na kuwa na kizazi kinachojiogopa na kuwajengea woga watoto na fikra za kikatili.

Mkazi mwingine wa Mtaa wa Jamhuri, Kata ya Miembeni, James Joackim, alisema kuwa ipo haja ya familia zenyewe kuanza kushtuka kuhusu mambo yanayoendelea na kuchukua hatua muhimu ya kudhibiti vitendo hivyo hatari kwa watoto.

"Ulinzi sio tu kuangalia amekula amelala au amevaaje la hasha, ulinzi ni kutenga muda wa kuongea naye na kutoa elimu yenye mifano, itasaidia mtoto atakapokuwa anacheza au yuko shuleni kukumbuka alivyoelekezwa na mzazi wake," alisema Joackim.

Ofisa Ustawi wa Jamii, Manispaa ya Bukoba, Japhet Kanoni alisema, zipo jitihada zinazofanywa na serikali kuifikia jamii na kutoa elimu ya kudhibiti ubakaji, ulawiti na manyanyaso, kwa kueleza madhara atakayopata mtendewa.

Alisema katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni, 2023, alipokea taarifa 17 za ukatili kwa watoto waliofanyiwa vitendo mbalimbali ikiwamo ulawiti, ubakaji, ambako vitendo vya ulawiti kwa jinsi ya Me ni 11 huku ubakaji kwa jinsi ya Ke wakiwa sita hali inayoonesha kuwa watoto wa kiume wapo kwenye hatari zaidi.

Kadhalika alisema, kati ya matukio 17, mashauri matatu yalifikishwa mahakamani na yanaendelea kusikilizwa huku mengine uchunguzi wake ukiwa bado unaendelea mahakamani.



Meneja Mkuu wa Kampuni ya CCECC Afrika Mashariki yenye kandarasi ya ujenzi wa Mradi wa Daraja la Magufuli na SGR, Zhang Junle kushoto akitoa ufafanuzi wa hatua mbalimbali za utekelezaji wa ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi maarufu kama daraja la J.P.Magufuli kwa wabunge walioambatana na Balozi wa China nchini, Chen Mingjian watatu kutoka kushoto (mbele) kukagua miradi inayotekelezwa na kampuni za kichina nchini. **PICHA:VITUS AUDAX**

# China, Tanzania kufungua ukurasa mpya ushirikiano

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BALOZI wa China nchini, Chen Mingjian, amesema taifa hilo litaendelea kupanua ushirikiano nchini utakaonufaisha pande zote katika maendeleo ya kijamii, uchumi wa kidijitali na nyanja zingine lengo likiwa ni kukuza ujenzi wa pamoja wa 'Ukanda na Barabara' hadi kiwango cha juu baada ya ufunguzi wa sura mpya ya ushirikiano wa kirafiki kati ya nchi hizo mbili.

Balozi Chen alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipotembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa Daraja Kigongo-Busisi, maarufu kama Daraja la JPM pamoja na Mradi wa Reli ya Kisasa SGR inayotekelezwa na kampuni ya CCECC kutoka nchini China.

Ziara hiyo iliyokuwa na lengo la kutembelea na kukagua miradi inatekelezwa na kampuni za kichina nchini iliwahusisha wabunge marafiki katika kikundi cha urafiki kati ya Bunge la Tanzania na China katika maadhimisho ya kumi ya mpango mkubwa wa kujenga kwa pamoja 'Ukanda na Barabara' uliopendekezwa mwaka 2013 na Rais wa China Xi Jinping na unaotambuliwa na jumuiya ya kimataifa.

Balozi Chen alieleza kuwa katika kipindi cha miaka kumi ya ushirikiano baina ya China na Tanzania maendeleo makubwa yameonekana kwenye sekta za usafirishaji wa anga, nchi kavu na baharini.

Kadhalika kasi na ubora wa biashara na uwekezaji kati ya China na Tanzania umeongezeka na biashara kati ya nchi hizo mbili kwa asilimia 250, na kufikia Dola za Marekani bilioni 8.31 mwaka 2022.

Vilevile, alisema kukua kwa miradi ya uwekezaji kwa zaidi ya Dola za Marekani milioni 100, kama vile, Koda Ceramics, Huaxin Mavini Cement, na Wangkang Float Glass, inayoelezwa kuleta kiasi kikubwa cha fursa za ajira kwa watu wa ndani na kukuza maendeleo ya pamoja.

"Tunaitaji kufungua sura mpya katika ushirikiano wetu kupitia Serikali ya Tanzania, Bunge, idara nyingine na marafiki kutoka tabaka mbalimbali za maisha ili kuongeza uhusiano imara baina ya nchi zetu na huu utakuwa mjadala muhimu katika kuadhimisha miaka 60 tangu kuanzishwa kwa uhusiano wetu kidiplomasia yatakayoadhimishwa mwaka kesho," alisema Balozi Chen.

Akizungumza kwa niaba ya wabunge marafiki kutoka Tanzania, Mbunge wa Jimbo la Masasi, Godfrey Mwambe alisema, lengo la urafiki huo ni kukuza uhusiano zaidi baina ya nchi hizo mbili ikiwa ni pamoja na kujifunza mbinu mbalimbali za kiteknolojia zinazofanywa na kampuni za kichina ili kuwezesha wazawa kuwa na uwezo wa kutekeleza miradi ya namna hiyo.

Kadhalika, alisema miradi hiyo imekuwa ikifuata utaratibu wa kuwatumia wataalamu wa ndani na kuwaacha na ujuzi ambao utalisaidia taifa katika hatua za kuanza kuwatumia wataalamu wa ndani katika utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Kwa mujibu wa Meneja Mkuu wa Kampuni yenye kandarasi ya ujenzi wa Mradi wa Daraja la Magufuli na SGR ya CCECC Afrika Mashariki, Zhang Junle, kampuni hiyo imeanza utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini kuanzia miaka ya 1960-1970 katika ujenzi wa reli ya TAZARA.

Ziara hiyo ya Balozi wa china ilifanyika katika Mkoa wa Mwanza unapotekelezwa mradi wa daraja kubwa lenye urefu wa kilomita tatu pamoja na barabara za kuunganisha daraja hilo pande mbili kwa kilomita 1.66. vilevile, katika Mkoa wa Shinyanga kilipo kituo kikuu cha ujenzi wa reli ya SGR kipande cha tano cha ujenzi wa reli hiyo ya kisasa yenye urefu wa kilomita 1,950.

# Tabora namba 5 duniani wagonjwa selimundu

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKOA wa Tabora umetajwa kuwa nafasi ya tano ulimwenguni kwa kuwa na wagonjwa wengi wa selimundu (sickle cell) kwa kuwa na 978 kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Tabora Kitete, Dk. Renatus Burashahu, alitoa taarifa hiyo wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari katika uelimishaji kuhusu ugonjwa huo.

Alifafanua kuwa katika mwaka 2022 kulikuwa na jumla ya wagonjwa 386 waliolazwa wodi ya watoto kwa sababu ya changamoto za kiafya za ugonjwa huo na wengine 291 kuhudhuria kliniki ya selimundu na 2023 kuanzia Januari hadi Mei, jumla ya wagonjwa 188 walilazwa, na 133 walihudhuria kliniki.

Alisema hali hiyo siyo nzuri na kuwahimiza waandishi wa habari mkoani humo kufikisha elimu ya kujikinga na ugonjwa huo wa kurithi ili kupinguza idadi ya wagonjwa endapo jamii itachukua tahadhari hususa wanandoa kupima kabla ya kuingia kwenye mahusiano.

Aidha, inakadiliwa kuwa asilimia 20 ya Watanzania wanabeba vinasaba vya ugonjwa wa selimundu ambao unaongezeka mwaka hadi mwaka katika Hospitali ya Rufani Kitete kutokana na idadi kuongezeko kwa wagonjwa wanaofika kupata huduma.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto Mkoa wa Tabora, Amon Ryakitimbo, aliishauri jamii kabla ya kufunga ndoa waende hospitali kupima ugonjwa wa selimundu ili kujua afya zao na kuepusha kupata watoto wenye tatizo hilo.

Alisema lengo kubwa ya kupima ni kujua tatizo la ugonjwa huo kama ni mbebaji wa kinasaba na kuna njia ya kujikinga kwa kufuata kanuni na taratibu za kitabibu.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI WA5 WAPYA WALIOKATISHA TAMAA EPL UK. 12-13



Cristiano Ronaldo akiifungia Al-Nassr moja ya mabao yake ya kichwa. **PICHA: MTANDAO**

# WACHEZAJI WANNE WENYE MABAO MENGI YA KICHWA

**LONDON,** England

UWEZO wa kufunga mabao ya kichwa huwapa washambuliaji makali kwenye medani ya soka. Ni ujuzi ambao unahitaji muda wa kipekee, uratibu na nafasi. Kwa hiyo, kichwa ni ujuzi ambao sio kila mshambuliaji anao.

Uwezo wa kufunga mabao ya kichwa hakika huongeza safu ya ushambuliaji ya mchezaji, na kuifanya kuwa isiyotabirika na kuwa na changamoto kwa mabeki kuwakaba kwa ufanisi. Washambuliaji wanaofanya vizuri katika kufunga mabao ya kichwa ni tishio kubwa katika safu ya ushambuliaji ya timu yoyote.

Wanafanya maisha kuwa magumu kwa mabeki kwani kila krosi au sehemu ya kuweka kwenye eneo la hatari inamaanisha hatari.

Hapa tunawatazama wachezaji wanne waliofunga mabao mengi kwa kichwa katika historia ya mchezo huo mzuri...

#### #4 Pele - Mabao 124

Pele ni mmoja wa wanasoka bora wa wakati wote. Alisifika kwa uwezo wake wa ajabu wa kufunga mabao na alikuwa mshambuliaji mahiri ambaye alichanganya ustadi, kasi na usahihi wa kufunga mabao kwa kiwango kikubwa katika maisha yake yote.

Ustadi wa Pele akiwa na mpira miguuni mwake ni hadithi tu na ustadi wake wa kuvutia na safu ya upigaji mashuti ni aina ya mambo ambayo wanasoka na mashabiki waliyafurahia zaidi.

Licha ya kutokuwa mrefu sana, Pele alikuwa na uwezo mkubwa wa kuweka kiwango cha kutisha ambacho kilimfanya kuwa tishio angani.

Usahihi wake wa kichwa na nguvu vilimuwezesha kufunga mabao mengi na kumfanya kuwa mmoja wa washambuliaji waliobobea katika historia ya mchezo huo. Pele amefunga mabao 124 kwa kichwa katika maisha yake ya soka.

#### #3 Carlos Alonso Gonzalez - Mabao 125

Carlos Alonso Gonzalez, anayejulikana sana kama "Santillana" anachukuliwa kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi ambao Hispania imewahi kuwa nao. Licha ya kuwa na urefu wa mita 175 tu, Santillana ni maarufu kwa ustadi wake wa ajabu wa kichwa.

Uwezo wake wa kuruka ulikuwa wa ajabu na alikuwa tishio mara kwa mara kwenye eneo la hatari, akifunga mabao 125 kwa kichwa katika maisha yake ya soka. Ubora wa mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid ulimfanya kuwa mwiba kwenye shingo ya mabeki na kuwa nyenzo muhimu kwa timu zake.

#### #2 Gerd Muller - Mabao 144

Gerd Muller anatajwa sana kuwa mmoja wa washambuliaji wakubwa katika historia ya soka. Alikuwa mmaliziaji hatari ambaye angeweza kufunga kwa mguu wowote, lakini ujuzi wake wa kupiga kichwa ndio uliomtofautisha na kuwa mshambuliaji kamili.

Kama wengine kwenye orodha hii, Muller hakuwa mrefu sana, akiwa na urefu wa mita 176. Lakini ilionekana kana kwamba alikuwa na 'springi' miguuni mwake kila aliporuka angani na kukutana na mpira wa kichwa. Ustadi wake wa kupanga nafasi na uwezo wa kuruka ulimruhusu kuwashinda mabeki warefu zaidi.

Muller pia alikuwa na uwezo wa kuzalisha nguvu nyingi nyuma ya vichwa vyake. Kama matokeo, hadithi ya Ujerumani ilikuwa tishio la mara kwa mara kutoka kwake. Ubora wake wa kupiga kichwa ulikwenda mbali sana katika kuimarisha hadhi yake kama mmoja wa wafungaji bora zaidi ambao mchezo huu umewahi kuwashuhudia.

#### #1 Cristiano Ronaldo - Mabao 145

Mshindi mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or, Cristiano Ronaldo ni mmoja wa wanasoka bora zaidi wa wakati wote. Pia bila shaka ndiye mfungaji bora zaidi katika historia ya mchezo huu. Ustadi wa Ronaldo ni mzuri na ana ustadi wa kiufundi.

Ronaldo anasifika kwa uwezo wake wa kupiga kichwa. Amewashangaza wapinzani, mashabiki na wachambuzi kwa kasi yake ya ajabu na uwezo wa kuzalisha nguvu na usahihi katika vichwa vyake.

Mwendo wa gwiji huyo wa Ureno ndani ya eneo la hatari na matarajio yake yanamfanya kuwa mchezaji mgumu kuweza kumkaba.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, pia ana hisia kubwa ya wakati na sifa hizi zote zimemsaidia kuwa kamili angani. Ronaldo amefunga mabao 145 kwa vichwa katika maisha yake ya soka hadi sasa.

## ISIKUPITE

Neymar amevunja rekodi ya raia mwenza, Pele kama mfungaji bora wa muda wote wa Brazil kwa timu hiyo ya taifa baada ya kufunga mabao mawili katika ushindi wa 5-1 dhidi ya Bolivia juzi. Hivyo, Neymar mwenye miaka 31, sasa anafikisha mabao 79 mawili zaidi ya Pele, akiwa ameyafunguka kutokana na mechi 125 alizoichezea Brazil. marehemu Pele yeye alifikisha mabao 77 baada ya mechi 92 kati ya mwaka 1957 na 1971.



NIPASHE JUMATATU SEPTEMBA 11, 2023





# WACHEZAJI WA5 WAPYA WALIOKATISHA TAMAA EPL



ANDRE ONANA

**LONDON,** England

MARA tu gharama ya usajili inapolipwa na mchezaji kununuliwa, timu zinatumaini kwamba zitapiga hatua na hazitakatishwa tamaa kabisa. Wachezaji wa hadhi ya juu, waliosajiliwa kwa fedha nyingi hukaribisha uchunguzi mwingi na wanasoka hujikuta wakiwa kwenye shinikizo kubwa mara baada ya uhamisho maarufu.

**Sababu zinazofanya klabu kulipa fedha nyingi kwa wachezaji ni kwamba wanatarajia watu kama hao kuja na kucheza kwa kiwango cha juu bila usumbufu mwingi.**

Kwa maelezo hayo, tuwaangalie wachezaji watano wapya ambao wamezikatisha tamaa klabu zao mpya tangu kusajiliwa kwao msimu huu...

### #5 Nicolas Jackson (Chelsea)

Itakuwa ngumu sana kutarajia Nicolas Jackson kuwa mfungaji bora wa Chelsea. Idadi yake ya mabao 13 kwenye mechi 38 katika mashindano yote akiwa na Villarreal msimu wa 2022-23, ulikuwa wa kuvutia kwa kijana huyo mwenye umri wa miaka 22, lakini haifurahishi sana kwa klabu yake mpya ya Chelsea.

Kwa hiyo, kumtarajia kubeba jukumu la kufunga mabao peke yake akiwa Chelsea ni jambo gumu. Jackson ameanza maisha ya kawaida sana pale Stamford Bridge, akifunga bao moja pekee katika mechi nne za Ligi Kuu England hadi sasa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal, hajaonekana kuwa mkali mbele ya lango na tayari ana hatia ya kupotezea timu yake nafasi nyingi nzuri. Kipigo chembamba cha bao 1-0 cha Chelsea kutoka kwa Nottingham Forest, kilimfanya kocha, Mauricio Pochettino, kuwataka washambuliaji wake kuwa waangalifu zaidi mbele ya lango.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo, Pochettino alisema:

"Leo, tulitengeneza nafasi, lakini tulishindwa kuzitumia vya kutosha katika tatu ya mwisho. Tunapaswa kufunga kama tunataka kushinda."

### #4 Mason Mount (Manchester United)

Ikiwa kuacha kucheza mara mbili na kusahaulika katika mechi zake mbili za kwanza za mashindano akiwa na jezi ya Manchester United haikutosha, mambo yamekuwa mabaya zaidi kwa Mason Mount sasa.

Mchezaji mpya wa United aliyesajiliwa kwa euro milioni 64 anatarajiwa kuwa nje ya uwanja angalau hadi mwisho wa Septemba baada ya kupata jeraha wakati wakifungwa na Tottenham Hotspur.

Uchezaji wake katika mechi dhidi ya Wolverhampton Wanderers na Spurs haukuwa mzuri. Mount alishindwa kutoa aina yoyote ya uimara katika safu ya kiungo na alisukumwa kirahisi kufanya makosa katika nafasi ya tatu ya mwisho pia.

Anapaswa kutafuta maisha yake ya soka msimu huu katika Klabu ya Manchester United, lakini dalili za awali hazitii moyo.

### #3 Andre Onana (Manchester United)

Manchester United walionekana kubadilishana seti moja hadi nyingine kwenye idara ya golikipa. Wakati pasi na usambazaji wa Andre Onana umekuwa wa ubora na uboreshaji mkubwa zaidi ya David de Gea, lakini pale United anahitaji kufanya zaidi.

Onana ameokoa hatari chache tu za ubora hadi sasa. Baadhi ya mabao aliyofungwa yamekuwa ya kichekesho.

Katika ushindi wa mabao 3-2 wa United dhidi ya Nottingham Forest, Taiwo Awoniyi aliipatia Forest bao la kuongoza dakika ya pili. Licha ya kutakiwa kutoka Onana aliendelea kukumbatia lango na kumpa Awoniyi uhuru wa eneo la hatari na akafunga kirahisi.

Jaribio lake hafifu la kuuzuia mpira nje ya lango lilisababisha Declan Rice kufunga bao la dakika za majeruhi kwa Arsenal Septemba 3, mwaka huu. Onana hakufanya lolote kufanya mambo kuwa magumu kwa Gabriel Jesus dakika chache baadaye baada ya mshambuliaji huyo kufunga ndani eneo la hatari.

Ameruhusu mabao nane katika mechi nne za Ligi Kuu England na umekuwa mwanzo wa kusikitisha sana kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Cameroon.

### #2 Moises Caicedo (Chelsea)

Licha ya kipaji chake chote, euro milioni 116 kila wakati ilionekana kama fedha nyingi kutumia kwa Moises Caicedo. Ana umri wa miaka 21 pekee na kuhamia klabu yenye hadhi ya Chelsea kwa shinikizo la bei kubwa lilikuwa pendekezo la kutisha.

Uchezaji wa Caicedo akiwa amevalia jezi ya Chelsea haujakuwa mzuri hadi sasa. Amekuwa mbovu katika safu ya kiungo na hakucheza vema katika mechi zao za kupoteza dhidi ya West Ham United na Nottingham Forest.

### #1 Kai Havertz (Arsenal)

Mashabiki wa Ligi Kuu England hawawezi kushituka sana kuhusu hili baada ya kumtazama Kai Havertz akihangaika kule Chelsea. Kulikuwa na maswali yaliyoulizwa kuhusu jukumu gani Havertz angecheza katika klabu yake mpya ya Arsenal walipomsajili mapema msimu huu wa majira ya joto.

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta bado anaonekana kuwaza hilo na hakika haijasaidia kasi ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani.

Anaonekana kupunguza kasi ya mashambulizi kwa "Washikabunduki' hao. Ilikuwa ni pasi yake iliyokosa nafasi iliyosababisha Marcus Rashford kuifungia Manchester United bao katika mechi yao Septemba 3.

Pia alikosa nafasi ya wazi ya kufunga bao aliposhindwa tu kuwasiliana vizuri na mpira ndani ya eneo la hatari la United.

Katika mechi nne za Ligi Kuu hadi sasa, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ameshindwa kutoa mchango wowote wa mabao.

Arsenal itatumaini kwamba Havertz anaweza kutatua matatizo yake hivi karibuni au si muda mrefu kabla ya kuonekana walifanya makosa kutumia euro milioni 75 kumsajili.

## Nukuu

"Nilimwambia Havertz, mambo ni magumu mwanzoni. Nilipokutana na mke wangu, mwanzoni ilikuwa vigumu kumshinda. Ilikuwa ngumu, ilibidi nijaribu kumtumia ujumbe, na kuendelea na kuendelea. Na mwisho aliposema 'ndiyo, tunaweza kuwa pamoja ...' ni nzuri. Kuwa na bidii na kuamua, nadhani ndivyo ilivyokuwa," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta akimtia moyo Kai Havertz, ambaye hajawa na wakati mzuri uwanjani tangu atue klabuni hapo.**



"Sidhani. Kwa sababu ya umri wake na kwa sababu, Kombe la Dunia linapowasili, atagundua kuwa yeye hayupo sawa. Atagundua hilo, ikiwa anataka kuwa huko, watadai kutoka kwake kama alipokuwa na umri wa miaka 20. Kwa sababu hizi, ninaamini kwamba hatakuwapo," **nyota wa zamani wa Argentina, Carlos Tevez, akifafanua kwamba ni kwa nini hatarajii kuwa Lionel Messi ataichezea timu yao ya taifa kwenye Kombe la Dunia la Fifa 2026.**



"Nilifurahi sana kwa mwaka aliokuwa nao kwa sababu aliishi pande zote mbili za sarafu. Alikwenda mbinguni na Timu ya Taifa yaArgentina, akashinda kila kitu katika miaka ya hivi karibuni, na akiwa na Paris aliishi kuzimu, tuliishi kuzimu, yeye na mimi," **Neymar alipoulizwa alijisikiaje kuhusu kumuona rafiki yake mkubwa Messi akinyanyua Kombe la Dunia akiwa na Argentina mwaka 2022.**






Kiungo mkabaji wa Taifa Stars, Mzamiru Yassin, akila sahani moja uwanjani na Himad Abdell wa Algeria, huku Dickson Job (kulia) akiwa tayari kutoa msaada, katika mechi ya mwisho ya Kundi F iliyochezwa mjini Annaba nchini humo Alhamisi iliyopita na kumalizika kwa suluhu.

# SABABU TANO TAIFA STARS KUFUZU AFCON HIZI HAPA

**Na Adam Fungamwango**

HAYAWI Hayawi, sasa yamekuwa, kwani Timu ya Taifa ya Soka ya Tanzania, Taifa Stars, imefuzu kwenda kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, zitakazofanyika Januari 13 hadi Februari 11, mwakani nchini Ivory Coast.

**Usiku wa Alhamisi, Stars iligangamala kwenye Uwanja wa Mei 19, katika mji wa Annaba, nchini Algeria na kulazimisha suluhu dhidi ya vinara wa kundi, Timu ya Taifa ya Algeria.**

Wakati filimbi ya kumaliza mechi hiyo ilipopulizwa, iliashiria kuwa Stars imemaliza Kundi F ikiwa ya pili kwa pointi nane ambazo moja kwa moja zimeipa tiketi hiyo, juu yake kukiwa na Algeria iliyomaliza na pointi 16.

Licha ya kushinda mabao 2-0 dhidi ya Niger katika Uwanja wa Marrakech nchini Morocco, bado hayakutosha kuiengua Stars kwenye nafasi yake ya pili kwa sababu ilimaliza ikiwa na pointi saba, hivyo kushika nafasi ya tatu, Niger ikiwa ya nne na pointi zake mbili.

Hii inakuwa ni mara ya tatu kwa Tanzania kufuzu fainali hizo tangu nchi hii ipate Uhuru mwaka 1961 na tangu kuanzishwa kwa michuano hiyo.

Mara ya kwanza ilikuwa ni Agosti 26, 1979 ilipofuzu kwa mara ya kwanza ugenini, Uwanja wa Dag Hammarskjold, Ndola nchini Zambia, ilipolazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya wenyeji.

Straika hatari wa Zambia wakati huo, Alex Chola, alipachika bao dakika ya nne, lakini dakika ya 90 wakati mashabiki wanaamini timu hizo zingekwenda kwenye mikwaju ya penalti, Peter Tino alisawazisha.

Stars ilifuzu kwa jumla ya mabao 2-1, baada ya mechi ya kwanza iliyochezwa Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru) kushinda bao 1-0, lililowekwa wavuni na kiungo mkabaji wakati huo, Mohamed Rishald Adolf na fainali zake zilichezwa 1980 nchini Nigeria.

Mara ya pili ilikuwa Machi 24, 2019 ilipotinga AFCON ikiwa nchini, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ilipoifunga Uganda Cranes mabao 3-0 na kucheza fainali zake mwaka huo huo nchini Misri.

Katika makala haya tunakuletea tano zilizochangia Stars kutinga tena fainali hizo...

**1. Mkakakati wa kocha Amrouche**

Hata alipochagua wachezaji wake, aliita wengi wenye asili ya kukaba kuliko kushambulia. Lengo la Kocha Mkuu wa Stars, Adel Amrouche, halikuwa kushinda mechi, bali kufuzu.

Wengi waliponda uteuzi wake, lakini alikuwa na mkakati wake kuwa anataka kwenda na wachezaji ambao watakuwa na faida hata pale ambapo hawana mpira.

**2. Mfumo alioutumia siku ya mechi**

Kwanza kabisa aliweka mabeki ambao hawana tabia ya kucheza au kuchezea mpira sana wanapokuwa kwenye eneo la hatari na hii ni kuhakikisha mpira unaondoka mara moja karibu na lango kila unapookolewa. Hapo akawaweka Bakari Mwanyeto na Ibrahim Hamadi 'Bacca'.

Upande wa pembeni akamwanzisha Dickson Job ambaye kiasili ni beki wa kati, lengo kubwa ni kuwasaidia wenzake katikati pale inapobidi. Upande wa pili kushoto akamchezesha Dismas Novatus ambaye kiasili ni kiungo wa kukaba, hivyo na yeye kuna wakati alikuwa anakwenda kuwasaidia wenzake katikati.

Pale kati kulikuwa na viungo wakabaji wawili, Sospter Bajana ambaye alikuwa haondoki sana nyuma pamoja na Mzamiru Yassin alikuwa anamsaidia na hata akipanda ni kidogo sana.

Simon Msuva, winga ambaye ana uwezo wa kurudi nyuma kusaidia beki kwa asilimia kubwa alikuwa anamsaidia Job kukaba kuliko kushambulia.

Kwenye winga ya kushoto akampanga Haji Mnoga ambaye kiasili ni beki wa kushoto, lengo ni kumsadia moja kwa moja Novatus.

Aliyebaki huru mbele ni Clement Mzize tu, lakini Kibu Denis alikuwa na kazi ya kuwafanya mabeki wa Algeria wasiwe huru na mpira miguuni ili wasiweze kupiga pasi sahihi, kazi ambayo aliifanya vizuri kwa kiasi kikubwa.

**3. Ahadi za Rais Samia**

Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, bado aliendelea na ahadi zake kama ilivyokuwa msimu uliopita alipokuwa akitoa pesa taslimu pale timu za klabu na taifa zilipokuwa zikicheza mechi za kimataifa.

Simba Day, Agosti 6, mwaka huu aliahidi kuendelea kutoa zawadi au motisha ya fedha pale timu za klabu na taifa zitakapofanya vema. Kabla ya hapo, Machi mwaka huu, wakati ikikaribia kucheza dhidi ya Uganda Cranes aliahidi kutoa Sh. milioni 500 kama Taifa Stars ingefuzu kwenda AFCON 2023.

Hii ilisababisha wachezaji kuonekana kucheza kwa nguvu, kujituma, ari na upambanaji, vitu vilivyoongezwa na motisha huo wa rais.

**4. Kutokuwa na Kamati za Hamasa**

Miaka kadhaa nyuma ilionekana kama vile Stars bila ya kuwa na kamati za ushindi pamoja na hamasa haiwezi kufanya chochote kile.

Ni kamati zilizokuwa zikilundika watu wengi wakiwamo wanasiasa na wasanii ambao kazi yao ilikuwa ni kusafiri na timu nchi mbalimbali, lakini mara nyingi haikuonekana kuleta tija yoyote, badala yake walikuwa wakiitia timu presha.

"Hamasa haijafanyika kama zile zilizofanyika kipindi kilichopita kwa sababu tulishauriwa sana , kwamba miongoni mwa mambo tunayokosea ni kuipa presha kubwa timu yetu," alibainisha Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma.

**5. Uganda kutocheza kwao**

Pamoja na yote, katika soka wakati mwingine kupata ushindi au kufanikiwa ni lazima pia kuwe na mapungufu ya mpinzani wako. Moja ya vitu ambavyo Stars imenufaika navyo ni Timu ya


Taifa ya Uganda kutocheza kwenye uwanja wake wa nyumbani, ikiwa na maana nchini kwao.

Viwanja vya Uganda havikupasishwa kuchezewa michuano hiyo kutokana na kushindwa kukidhi vigezo, hivyo viko kwenye matengenezo.

Kwa maana hiyo mechi tatu za nyumbani ambazo Uganda ilitakiwa kucheza kwao imecheza kwenye viwanja tofauti nje ya nchi hiyo.

Hali hii inawezekana kabisa ikawa imechangia Stars kupata pointi tatu ilipocheza dhidi ya Uganda nchini Misri.

**JE, WAJUA?**



MARTA Vieira da Silva, ndiye anayeshikilia rekodi ya mabao mengi kwa Timu ya Taifa ya Wanawake ya Brazil, akiwa amecheka na nyavu mara 122 katika mechi 189 alizoichezea.



# ‘Miradi ya TBA izingatie thamani ya fedha’

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), ameagiza wakala huo kusimamia na kujenga majengo yenye ubora yanayoendana na thamani ya fedha ili kuendelea kuzivutia taasisi za ndani na nje ya nchi.

Dk. Ombeni Swai alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya bodi hiyo kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na wakala huo katika Mji wa Serikali Mtumba jijini hapa.

Alisema TBA ni lazima ihakikishe inaendelea kujenga majengo yenye ubora na ya mfano.

“Serikali ione kwamba thamani ya fedha iliyowekeza hapa inapatikana katika ubora, lakini pia utaalamu unaotumika uwe ni wa hali ya juu hata baada ya majengo kukamilika yaendelee kubaki na ubora wake kwa muda mrefu,” alisema.

Pia aliitaka kuendelea kutumia wataalamu wa ndani kwa kuwaamini na kuwajengea uwezo ili TBA ijenge majengo mengi na makubwa na kuitwa hata nje ya Tanzania kufanya kazi hiyo.

**Alimwomba Rais kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kumalizia majengo ambayo yako nyuma kiutekelezaji.**

Akizungumzia ukaguzi wa majengo uliofanywa na bodi hiyo, Dk. Swai alisema ujenzi wa ofisi za Wizara ya Kilimo na Wizara ya Afya ambao wanasimamia TBA, unaendelea vizuri kwa viwango stahiki.

“Katika jengo la Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sisi ndiyo tunajenga na ujenzi umefikia asilimia 93. Zimebaki kazi ndogo za kumalizia.

“Kwa ujumla, miradi inakwenda vizuri. Tuna imani kwa jinsi ambavyo serikali inaendelea kutoa fedha, (miradi) itakamilika kwa wakati,” alisema.

Alimwomba Rais kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kumalizia majengo ambayo yako nyuma kiutekelezaji.

Mkadiriaji Majenzi, Neema Kifua kutoka Idara ya Ushauri TBA, alisema katika Mji wa Serikali Mtumba, TBA inasimamia ujenzi wa majengo 17. Kati yake, 13 ni ofisi za wizara na manne ni ya ofisi za taasisi za serikali.

## Daktari Bingwa ahimiza wenza kupima afya kukabili sikoseli

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ILI kukabiliana na ongezeko la watoto wanaozaliwa na ugonjwa wa sikoseli nchini, wenza wameshauriwa kupima afya zao kabla ya kufunga ndoa ili kubaini kama wana vinasaba vya ugonjwa huo.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu na Kansa kwa Watoto Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Shakilu Juma, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki jijini hapa alipowasilisha mada wakati wa semina kwa waandishi wa habari kuhusu athari za ugonjwa huo katika jamii.

Alisema licha ya juhudi nyingi za kupunguza makali ya ugonjwa huo, bado hali ni mbaya na watoto wengi kuendelea kuteseka kutokana na uelewa mdogo wa wazazi kuhusu namna ya kuepuka mazingira yanayoweza kuchochea hali hiyo.

Dk. Jumanne alihadharisha kuwa ndoa za watu wenye vinasaba vyenye ugonjwa huo zinachochea watoto kuzaliwa na ugonjwa wa sikoseli kwa kuwa wote wanakuwa na vichocheo vya kurithi.

Akieleza ukubwa wa tatizo hilo, bingwa huyo alisema Tanzania ni nchi ya tano kwa kuwa na watoto wengi wanazaliwa na ugonjwa wa sikoseli.

“Kila mwaka nchini watoto 14,000 huzaliwa na ugonjwa huu huku watoto 10,000 kati yao huzaliwa mikoa ya Kanda ya Ziwa. Kwa Mkoa wa Mwanza tu, wanazaliwa watoto 1,700 kwa mwaka mwenye tatizo hili,” alisema.

Kuhusu matibabu ya ugonjwa huo, bingwa huyo alisema yanafanyika kwa kupandikiza uloto kutoka kwa ndugu wa karibu kwenda kwa mtoto mwenye tatizo.

“Matibabu ya sikoseli ni ghali hususani katika kupandikiza uloto ambapo kwa mgonjwa mmoja, huduma hii huweza kugharimu kiasi cha Sh. milioni 30 hadi 40, jambo ambalo ni gumu kwa Watanzania wenye maisha duni.

“Hivyo, ili kuepuka haya lazima jamii ikubaliane kupima kabla ya ndoa ili kuwaepusha watoto wetu maumivu wanayopitia,” alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sikoseli, Wizara ya Afya, Dk. Asteria Mpoto, alisema serikali inafanya jitihada kuweka unafuu katika huduma za sikoseli ikiwa ni pamoja na kuimarisha matibabu ya kibingwa ya kupandikiza uloto.

Alisema kwa kuanzia serikali imeanza kugharamia matibabu ya kibingwa kwa watoto wenye ugonjwa huo kwa kupatindikiza uloto ili kuwapunguzia maumivu wanayoyapata.



Jengo la soko la Bahi wilayani Bahi likionekana kuwa wazi kutokana na kukosa wafanyabiashara waliokuwa wamekadiriwa kufanya biashara ambao ni zaidi ya mia tatu baada ya kutelekezwa na Halmashauri kwa kushindwa kulikamilisha kwa miaka kumi na tano toka lijengwe. **PICHA: PETER MKWAVILA** .

# Madiwani watakiwa kuwa mabalozi wa usalama, afya

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Cyprian Luhemeja, amewataka madiwani wa Mkoa wa Dodoma kuwa mabalozi wa usalama na afya katika miradi yote wanayoisimamia na inayotekelezwa kwenye kata zao.

Lengo ni kulinda nguvu kazi dhidi ya magonjwa na ajali katika maeneo ya kazi.

Luhemeja alitoa rai hiyo jana jijini hapa alipofunga mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi yaliyoandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa madiwani wa viti maalum na wajasiriamali wanawake wa mkoa huo yaliyokwenda sambamba na upimaji afya.

Alisema mkoa huo kwa sasa una miradi mingi inayotekelezwa na serikali ikiwamo ya ujenzi, maji, barabara, upanuaji wa mji, hivyo kuwapo haja ya kuweka mifumo thabiti ya kumlinda mfanyakazi dhidi ya vihatarishi vya magonjwa na ajali zitakazotokea wakati wa utekelezaji wa miradi.

Aliitaka OSHA kuendelea kutoka mafunzo hayo kwa maeneo mengine ili kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa salama wakati wote wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Dodoma na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatuma Toufiq, alisema mafunzo hayo kwa madiwani yamekuja muda mwafaka kutokana na wingi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

“Ninawapongeza sana waheshimiwa madiwani wote kwa mafunzo haya ambayo mmeyapata. Ninatarajia kuwa mtakaporudi katika maeneo yenu ya kiutendaji, mtakuwa mabalozi wazuri wa kuitangaza OSHA kwamba kazi wanayoifanya ni kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya wafanyakazi wote katika maeneo ya kazi.

“Serikali imekuwa inatoa fedha nyingi za maendeleo katika mkoa wetu na kuna miradi mingi inatekelezwa ikiwamo ya ujenzi wa barabara, ujenzi wa reli ya kisasa na bomba la mafuta.

“Miradi hii inapita kwenye maeneo yetu, hivyo sisi madiwani ni wajibu wetu kusimamia hilo ili fedha hizo zinazoletwa kwetu zilete tija,” alisema.

Akizungumza kwa niaba ya madiwani hao, Mwanaharusi Bata, aliipongeza OSHA kwa kuendesha mafunzo hayo na kuahidi watаifikisha elimu hiyo ya usalama na afya walioipata katika miradi mbalimbali inayotekeleza katika maeneo yao wanapotoka.

Awali, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema lengo kubwa la mafunzo haya ni kuwaelimisha madiwani hao kuhusu majukumu mbalimbali ya OSHA ili wanapopitisha na kusimamia miradi mbalimbali ya kimaendeleo waweze kushirikiana na OSHA katika kulinda nguvu kazi kwa kuboresha mifumo ya usalama na afya katika miradi hiyo.

“Mafunzo haya ni sehemu ya maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu na tutahakikisha tunaendelea kutoa elimu na kuyafikia makundi mbalimbali na moja wapo ni hili la watunga sera ili inapotokea wanakaa katika mabaraza ya kupitisha miradi, basi waangalie miradi hiyo kama imekidhi viwango vya usalama na afya kama sheria husika inavyoelekeza,” alisema.





# Udumavu waundiwa mkakati kutokomezwa

**Na Nebart Msokwa,**
RUNGWE

UONGOZI wa Mkoa wa Mbeya umeanzisha mkakati maalum wa kukabiliana na udumavu kwa kujenga vituo maalum vya kulelea watoto wenye umri wa chini ya miaka miwili hasa katika maeneo yenye shughuli za kiuchumi zinazofanywa na wanawake.

Vituo hivyo vinatajwa kusaidia wanawake wanaofanya kazi kwenye maeneo hayo kuwapatia watoto wao chakula kwa wakati na kuwaruhusu kucheza michezo mbalimbali changamshi ili kuimarisha afya zao.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipomwakilisha Mkuu wa Mkoa, Juma Homera katika maadhimisho ya Siku ya Lishe Duniani ambayo kimkoa yalifanyika katika Kijiji cha Mpandapanda, wilayani Rungwe.

Malisa alisema mkoa huo unalenga kuanza na vituo vinne katika wilaya na halmashauri nne tofauti ambazo zina shughuli mbalimbali za uzalishaji mali zinazofanywa na wanawake.

Alizitaja wilaya ambazo wanakusudia kuanza nazo kuwa ni: Chunya ambayo wanawake wanashiriki kwenye machimbo ya dhahabu na kwenye kilimo; Mbarali ambako wanashiriki kilimo cha mpunga; Rungwe na Mbeya ambako wanawake wanashiriki kilimo na biashara.

"Wanawake wanaofanya shughuli kwenye maeneo haya watatumia vituo hivyo kuwalisha watoto wao kwa wakati sahihi ili kukabiliana na udumavu, lakini vituo hivi vitawapa watoto nafasi ya kucheza na kufanya matendo changamshi yatakayochochea ukuaji wao," alisema Malisa.

Mwakilishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya lishe, Dk. Jim Yonazi, alisema serikali imeandaa miongozo mbalimbali kwa wadau wa lishe kote nchini kwa lengo la kuhakikisha taifa linakuwa na watu wenye afya bora.

Alisema mwongozo unaotekelezwa kwa sasa unamtaka kila mdau anayeshiriki kwenye masuala ya lishe anakuwa na nia thabiti ya kukabiliana na mambo ya lishe hasa kwa watoto.

Alisema Ofisi ya Waziri Mkuu itahakikisha inashirikiana na wadau wote kuhakikisha suala la lishe kwa watoto linapewa kipaumbele ili kutokomeza kabisa tatizo la udumavu na mambo mengine yanayotokana na lishe duni.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Huduma kwa Watoto (UNICEF) Tanzania, Elke Wish, alipongeza serikali kwa kuanzisha mkakati wa lishe ambao unaeleweka na unatekelezwa katika ngazi mbalimbali.

Alisema mkakati huo unatafsirika vizuri kuanzia katika ngazi ya kitaifa mpaka kwenye maeneo ya vijijini ambako hasa ndiko utekelezaji wake unafanyika.

Aliwataka wadau mbalimbali kuendelea kutekeleza mkakati huo ili kutokomeza kabisa tatizo la udumavu kwa watoto na kufanya taifa kuwa na watu wenye uwezo mkubwa wenye uzalishaji.

Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) katika masuala ya lishe, Afshan Khan, alisema Wilaya ya Rungwe ina kila aina ya chakula ambacho kikitumika vizuri kinaweza kusaidia kutokomeza udumavu.

Alisema vyakula vinavyopatikana katika wilaya hiyo havipatikani kirahisi maeneo mengine na hivyo kuwataka wenyeji kuvitumia vizuri.

Licha ya Mkoa wa Mbeya kuwa miongni mwa mikoa inayozalisha chakula kwa wingi, ni miongoni mwa mikoa yenye kiwango kikubwa cha udumavu kwa watoto, hali inayotajwa kusababishwa na ulaji usiokuwa sahihi.



Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu (kulia) akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa jana asubuhi katika kijiji cha Simambwe baada ya kukamilisha mbio zake katika wilaya hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Polisi watoa angalizo wanandoa kufanya 'doria' simu ya mwenza

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Dawati la Jinsia Mkoa wa Njombe, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Wilfred Willa, amewataka wanandoa kuacha mtindo wa kufanya upekuzi katika simu za wenza wao ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea ikiwamo mauaji na kuvunjika kwa ndoa.

Akizungumza wakati wa kutoa elimu katika Mtaa wa Ngalanga, Halmashauri ya Mji Njombe mwishoni mwa wiki, Willa alisema moja ya vyanzo vya migogoro ya ndoa ni kufanya 'doria' zisizo na ulazima katika simu ya mwenza.

Alisema matokeo ya doria hizo huwa watu kujinyonga, kufanyiwa ukatili na kuvunjika kwa ndoa, hali inayofanya ongezeko la watoto wanaolelewa na upande mmoja.

"Katika simu watu wameuana, watu wamekunywa sumu, watu wamejinyonga, watu wameshikiana mapanga, watu wamegombana, familia zimetetereka, watoto hawapelekwi shuleni" alionya.

Willa alisema elimu hiyo ni sehemu ya mwendelezo wa utoaji elimu ya kukabiliana na kudhibiti ukatili wa kijinsia kwa lengo la kuwa na jamii yenye upendo, maadili na heshima baina yao.

"Pamoja na yote hayo, suala la imani za kishirikina ikiwamo ramli chonganishi ni miongoni mwa mambo tunayokemea kila kukicha. Na hii nayo ni moja kati ya vyanzo vikuu vya mauaji katika mkoa wetu wa Njombe," alisema Willa.

Wakazi wa Njombe walishukuru kwa elimu iliyotolewa huku wakiahidi kuifanyia kazi na kuwa mabalozi wazuri wa kuendeleza maadili mema kwa manufaa ya sasa na baadaye.

"Elimu tumeipokea, ni wajibu wetu sasa kuacha kuviziana, maana wakati mwingine upo unaoga unashangaa mtu anavizia simu yako," alisema Enesia Njavike. Jovina Tweve alisema elimu hiyo inasaidia pia kujikumbusha na ili kuondokana na mambo maovu.

"Ifike mahala sasa mkichokana mwachane kwa maelewano ili mwendelee kushirikiana kulea watoto na sio kuchukua uamuzi wa kumpoteza mwenza wako," alishauri Tweve.

Mkoa wa Njombe ni miongoni mwa mikoa ambayo kwa miaka ya karibuni imekuwa inakabiliwa na ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ikiwamo mauaji na ubakaji.

## Halmashauri yaja na uji maalum kuzuia utapiamlo na kiribatumbo

**Na Nebart Msokwa,**
BUSOKELO

HALMASHAURI ya Busokelo mkoani Mbeya imeanzisha programu maalum ya kuwapatia uji lishe watoto chini ya miaka mitano kila baada ya miezi mitatu ili kuwakinga dhidi ya utapiamlo na kiribatumbo.

Vilevile, imeanzisha programu ya utoa elimu kwa wajawazito na wazazi kuhusu masuala ya lishe wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua ili kuhakikisha wanashiriki mapambano dhidi ya matatizo hayo.

Ofisa Lishe wa Halmashauri hiyo, Mwanahawa Ntanda, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati Mwenge wa Uhuru ulipozindua Zahanati ya Bwibuka iliyoko katika halmashauri hiyo. Alisema utaratibu huo unatekelezwa katika maeneo yote.

Alisema mbali na kutoa uji lishe, pia wanaandaa chakula chenye mchanganyiko wa aina mbalimbali ya lishe kwa ajili ya kuwasaidia wajawazito kuwa na afya bora.

"Hii ni programu endelevu, afya na lishe haishii kwa watoto pekee, bali hata kwa wanawake wajawazito. Tunachofanya ni kuwapa vyakula mchanganyiko, huwa tunawachanganyia aina nne ya vyakula," alisema Mwanahawa.

Baadhi ya wanawake waliokuwa wanapewa huduma katika zahanati hiyo waliishukuru serikali kwa kuanzisha utaratibu huo wakieleza kuwa unawasaidia kuimarisha afya zao na za watoto wao huku wakipata pia elimu ya namna ya kuandaa vyakula hivyo.

Mmoja wa wanawake hao, Maria Mwangoka, alisema wananufaika na programu hiyo ambayo huwasaidia kupata elimu ya afya hususani matumizi ya vyakula kwa wajawazito na watoto.

"Mimi binafsi mwezi Julai mwanzoni nilikuja hapa, nilipata huduma na leo tena tumekuja kupata huduma hi. Kuna mambo tulikuwa hatuyajui, lakini wataalamu wetu wametuelimisha vizuri na kila tunapokuja wanatuelimisha vizuri," alisema Mariam.

Zahanati hiyo itawanufaisha zaidi ya wakazi 1,600 wa vijiji vya Bwibuka na Ntapisi ambao walikuwa wanatembea umbali wa zaidi ya kilomita sita kutafuta huduma.

Mwenge wa Uhuru umehitimisha ziara yake katika Halmashauri ya Busokelo na jana asubuhi ulikabidhiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na leo unatarajiwa kuingia jijini Mbeya.



## Watetezi haki wanyama, ndege wakwamisha mradi uteketezaji kunguru waharibifu mazao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKULIMA wa Shehia za Fojoni, Zingwezingwe na Kiombamvua Bumbwini, Mkoa wa Kaskazini Unguja Visiwani Zanzibar wameiomba serikali kudhibiti ongezeko la ndege aina kunguru wanaofanya uharibifu wa mazao yao mashambani.

Waliyasema hayo katika mkutano maalum kati ya wananchi na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwa ni utaratibu wa mkuu huyo wa kusikiliza kero za wananchi katika shehia na kuzitafutia ufumbuzi.

Alhaji Abdallah Mgeni, miongoni mwa wakulima hao, alisema ndege huyo huvamia mashamba yao na kuharibu kabla ya kuvunwa.

Alisema uharibifu huo huwasababishia hasara na kutonufaika na kilimo wanacholima ikiwamo mahindi, nyanya na mazao mingine.

"Hakuna tunachokipata katika kilimo wala katika mifugo maana kunguru hula mpaka vifaranga vya kuku pamoja na mayai, kwa kweli tushachoka nao tunaomba nguvu za ziada kutoka serikalini kuangamizi kunguru," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alimwagiza Ofisa Kilimo wa mkoa huo kutoa ufafanuzi kuhusu ndege hao kwa kuwa serikali ilikuwa na mradi maalum wa kutokomeza kunguru.

"Afisa kilimo haya tupe ufafanuzi wa jambo hili maana nakumbuka serikali ilikuwa na mpango maalum wa kutokomeza kunguru kutokana na uharibifu na kuchafua mazingira," alisema Ayoub.

Ofisa Kilimo, Juma Kona Mosi, alikiri kuwa serikali ilikuwa na mradi wa kutomomeza wadudu waharibifu ikiwamo kunguru, lakini umesita baada ya kuibuka kwa malalamiiko ya watetezi wa haki za wanyama na ndege.

"Miongoni mwa malalamiko yaliyoibuka kutoka kwa watetezi wa haki za wanyama na ndege kuwa viumbe hivyo vina haki ya kuishi kama wanyama wengine hivyo sio busara kuwaua," alisema.

# Mwinyi aahidi kuyafanyia kazi mapendekezo haki jinai

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameahidi kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Maboresho ya mifumo ya Taasisi za Haki Jinai ambayo itatoa mwangaza kwa Serikali ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuboresha mifumo na taasisi zinazohusiana na masuala hayo kwa nia ya kupatikana haki kwa ufanisi.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipokutana na Tume hiyo iliyoongozwa na Mwenyekiti Jaji mstaafu, Mohamed Othman Chande na Makamu Mwenyekiti, Balozi Ombeni Sefue, walipomkabidhi ripoti yao.

Dk. Mwinyi alisema serikali zote mbili SMZ na SMT imeyapokea mapendekezo hayo na kuahidi kuyafanyia kazi kwa kina ili kuleta mabadiliko na mageuzi makubwa kwa nia ya kupatikana kwa haki nchini.

Alisema utekelezaji wa mapendekezo hayo kwa kiasi kikubwa unaendana na kutegemeana na taasisi zote za haki jinai za Bara na Zanzibar.

Rais Mwinyi alizungumzia ushirikiano mzuri uliopo baina ya Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa ya Zanzibar (ZAECA) na ya kupambana na dawa za kulevya, zimepata msaada wa kujengewa uwezo na wenzao kutoka Bara kwa kupewa mafunzo.

"Bila shaka ni sahihi kabisa lazima kuwe na kubadilishana ujuzi na uzoefu, ushirikiano wa karibu," alisema.

Kuhusu mahakama ya rufani kufanya kazi zake Zanzibar, alisema tayari suala hilo linashughulikiwa pamoja na kuisifu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongeza nguvu kwenye ujenzi wa miundombinu ya Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Mwenyekiti Chande, alisema Tume ilifanikiwa kuzifanyia kazi changamoto za taasisi 15 zilizopendekezwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zikiwamo Jeshi la Polisi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Magereza.

Taasisi nyingine ni Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Mahakama ya Tanzania, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu Uhamiaji, Mkemea Mkuu wa Serikali na taasisi nyengine zinazohusu masuala ya jinai kwa kutathmni ushirikiano wa taasisi hizo na kuangalia nidhamu, mifumo ya ajira, viwango vya weledi, tume ya upandishaji vyeo, ufanisi mahusiano, nidhamu, ufanisi matumizi ya teknolojia na motisha.





Baadhi ya wananchi wa kijiji cha Fujoni wakimsikiliza mkuu wa mkoa wa kaskazini Unguja, Ayoub Mahmoud ambae hayupo pichani wakati akitoa ufafanuzi wa kero za wananchi katika muendelezo wa mikutano yake ya kusikiliza kero kwa kila shehia mkoani humo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# Petroli yashuka bei, dizeli na mafuta ya ndege yapaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BEI ya mafuta ya petroli imeshuka kwa mwezi huu wa Septemba huku dizeli na mafuta ya ndege ikiongezeka.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), bei ya dizeli na mafuta ya ndege imeongezeka kwa sababu ya kupanda kwa bei ya nishati hiyo duniani.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Meneja Uhusiano ZURA, Mbaraka Hassan Haji, alisema bei hizo zimeongezeka kwa asilimia 21 na gharama za bima na usafirishaji kwa asilimia 62 ikilinganishwa na mwezi uliopita.

Akizitaja bei hizo alisema, mafuta ya dizeli kwa mwezi huu yanauzwa kwa Sh. 3,012 kutoka Sh. 2,843 ya mwezi uliopita tofauti ya Sh. 169 sawa na asilimia 5.94.

Kwa mafuta ya ndege alisema mwezi huu yanauzwa kwa Sh. 2,448 ikilinganishwa na mwezi uliopita ambayo yaliuzwa kwa Sh. 2,365 ambayo imeongezeka kwa Sh. 83 sawa na asilimia 3.51.

Aidha petroli kwa mwezi huu imeshuka kutoka Sh. 2,970 hadi Sh. 2,950 huku mafuta ya taa yakibaki kwa bei ile ile ya Sh. 2,921.

Hata hivyo, alisema ZURA hupanga bei hizo kwa kuzingatia mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani, gharama za uingizaji mafuta katika bandari ya Dar es Salaam na Tanga, thamani ya Shilingi ya Tanzania kwa dola, gharama za usafiri, bima na premium hadi Zanzibar, kodi na tozo za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Alisema nishati hiyo ipo ya kutosha na kwamba hakuna sababu ya wananchi kuingia hofu kutokana na upatikanaji wake katika vituo vyote vya mafuta vilivyokuwapo Unguja na Pemba.

Pia alisema Mamlaka inaendelea kufatilia na kudhibiti soko la mafuta na bei zake kwa ukaribu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha bei za bidhaa hizo haziongezeki maradufu na kutokea athari katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

# Profesa Makulilo aona shida akili bandia machapisho ya kitaaluma

**Na Miraji Msala**

MAENDELEO ya Teknolojia yamekuja na manufaa makubwa, lakini katika uandishi wa kazi za kitaaluma yameleta changamoto nyingi ikiwamo utengenezaji wa machapisho kupitia akili bandia kunakofanywa na baadhi ya watu wasio waaminifu.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) Anayesimamia Teknolojia za Kujifunzia na Huduma za Mikoa, Prof. Alex Makulilo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozindua mafunzo ya uhariri kwa wahariri wakuu wa majarida ya kitaaluma ya OUT yaliyofanyika katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere, wilayani Kibaha, mkoani Pwani.

Prof. Makulilo alisema kwa sasa teknolojia imerahisisha upatikanaji wa machapisho ya kujisomea kupitia mitandao mbalimbali na pia kurahisisha ufanyikaji wa utafiti mbalimbali.

Hata hivyo, alisema kuna watu ambao si waamnifu wanaweza kutumia akili bandia kutengeneza machapisho na kuwafanya waonekane wana uwezo mkubwa wa kufanya utafiti na kutoa machapisho mengi kwa mwaka ilhali hawajafanya utafiti. Ni akili bandia ndiyo iliyofanya kazi ya kuzalisha machapisho hayo.

"Akili bandia ina uwezo wa kuzalisha andiko au hata kitabu. Hii imelazimisha baadhi ya taasisi za elimu ya juu kutoa angalizo kwa wanataaluma na wanafunzi kukiri kama kazi wanazotoa ni za kwao au wamezipata kupitia akili bandia.

"Hili hufanyika kupitia mfumo maalum unaojulikana kama Plagiarism Checker. Hivyo, katika mfunzo haya, moja ya mjadala uwe ni namna ambavyo ninyi wahariri mnavyoweza kukabiliana na tatizo hili linalotokana na maendeleo ya teknolojia," alisema Prof. Makulilo.

Alisema kinachofanya nchi nyingi za Afrika kuwa nyuma katika utafiti na kutoa machapisho yaliyo bora ni ufinyu wa bajeti za utafiti.

Alisema serikali nyingi barani Afrika zinatenga bajeti ndogo au kutotenga kabisa bajeti za utafiti, jambo linalofanya watafiti kujigharamia wenyewe kwa fedha kidogo walizonazo na hivyo kutofikiwa kwa ubora wa utafiti na machapisho yatokanayo na utafiti huo.

Mkurugenzi wa Utafiti, Machapisho na Ugunduzi wa chuo hicho, Dk. Harrieth Mtae, alisema kwa sasa kuna uhitaji mkubwa wa majarida kwa ajili ya kupokea machapisho kutoka kwa wanataaluma na watafiti.

"Hii ni kutokana na Serikali ya Tanzania kuhamasisha ufanyaji wa utafiti vyuoni ikijumuisha wahadhiri na wanafunzi. Hata hivyo, pamoja na uhitaji huo kuwa mkubwa, bado utokaji wa machapisho hayo umekuwa ukisuasua.

"Haya mafunzo ni katika kuboresha majarida yaliyopo chuoni. Chuo hiki kina majarida saba, lakini utokaji wake umekuwa siyo katika mpango wa vipindi au muda wa utokaji unaotakiwa.

"Hivyo, mafunzo haya yametukutanisha wahariri wote ili kuona wapi panatukwamisha ikizingatiwa uhitaji wa watu kutoa machapisho ni mkubwa sana," alisema Dk. Mtae.

Mkurugenzi wa Shahada za Juu za OUT ambaye pia ni Mhariri Mkuu wa Jarida la Huria, Prof. Magreth Bushesha, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwao kwa kuwa yanakwenda kutatua changamoto ambazo wamekuwa wanakutana nazo katika kuhudumia majarida yaliyopo.

Mwezeshaji wa Mafunzo hayo, Prof. Lazarus Makewa, alisema wanatoa mafunzo hayo ili kuyafanya majarida yote kuwa hai na kazi za kitaaluma zichapishwe kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

Mafunzo hayo ya uhariri kwa wahariri wa majarida ya OUT yaliyoandaliwa na Kurugenzi ya Utafiti, Machapisho na Ugunduzi, yalifanyika kwa siku mbili kuanzia Septemba 6 mwaka huu katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere, wilayani Kibaha.



Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Mohamed Ali Ahmed (katikati) akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu Mkutano Maalum wa Baraza la Vyama vya Siasa, utakaofanyika kesho (jumatatu) jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere ambapo Rais Samia Suluhu anatarajiwa kufungua mkutano huo. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Habari na Elimu kwa Umma, Abuu Kimario na kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Sheria, Muhidini Mapeyo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## RUWASA yatakiwa kupeleka maji sekondari ya wasichana

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), mkoani hapa, wametakiwa kupeleka huduma Shule ya Sekondari ya Wasichana, masomo ya Sayansi, kuwaepusha kutembea mwendo mrefu kufuata maji.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, alitoa amri hiyo, wakati anakabidhi kwa Wakala huyo shehena ya mabomba ya maji, yaliyopelekwa kufanya kazi ya kusambaza huduma hiyo Kata ya Kilangala, Tarafa ya Mchinga, Manispaa ya Lindi.

Sekondari hiyo ina idadi ya wanafunzi 80 iliyoanzishwa Julai, mwaka huu.

Akizungumza na watendaji pamoja na wakazi waliojitokeza katika makabidhiano hayo, Ndemanga alisema serikali imedhamiria kuwaondolea wananchi upatikanaji huduma ya maji wakimo wa Kata ya Kilangala na kwamba ni vizuri ikafikishiwa huduma hiyo kwa haraka.

Alisema kutokana na umuhimu wa uhitaji wa maji ameipa Wakala huyo wiki mbili kukamilisha kazi ya kupeleka huduma katika sekondari hiyo masomo ya Sayansi iwe imekamilika.

Alitaka mabomba hayo yatumike kwa kazi iliyokusudiwa na si vinginevyo, huku akiwasisitiza wananchi kuwa walinzi wa mali walizopelekewa zisichukuliwe na watu wengine kwa ajili ya kujinufaisha kinyume na ilivyopangwa.

Akipokea mabomba hayo yatakayotumika kusambaza maji umbali wa kilomita 19 ya mradi huo utakaohudumia vijiji vitatu vya kata hiyo, Meneja wa RUWASA, Wilaya ya Lindi, Iddi Pazi, aliahidi kutekeleza maagizo yake kabla ya muda waliopewa.

# Mashirika yasiyo ya kiserikali Pwani yapewa angalizo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KAIMU Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Savera Salvatory, amesema serikali ya mkoa huo inategemea kuona mashirika yasiyo ya kiserikali yakitekeleza wajibu wao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kwa kutoa taarifa zitakazokuwa chachu ya kuboresha utendaji kazi wao.

"Sitegemei katika mkoa huu kuwapo kwa mashirika ya mfukoni yanayotumia simu za mkononi yasiyo na ofisi na yale ya kifamilia yanayofanya kazi kwa lengo la kujinufaisha," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Kaimu Katibu Tawala huyo, mkoa huo una mashirika zaidi ya 300 yanayofanya kazi katika halmashauri tisa na hadi Septemba mwaka huu ni mashirika 82 pekee yanayofanya kazi kikamilifu.

Salvatory aliyasema hayo juzi mjini Kibaha alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa mashirika yasiyo ya kiserikali na kuyasisitiza kufanya kazi kwa uwazi, ukweli, ushirikiano kwa kuhakikisha fedha za miradi zinatumika kama zilivyopangwa kwa lengo la kusaidia wananchi.

"Utendaji kazi wa mashirika zaidi ya 218 sio wa kuridhisha kwa kuwa hamuwasilishi taarifa za fedha na utekelezaji wa miradi kwa wakati ilhali mkitambua ni wajibu wenu na sheria inawataka kufanya hivyo, kwa hali hiyo mkoa unashindwa kuwatathmini kwa kukosa taarifa."

"Pia, sitarajii kuona wala kusikia kama kuna mashirika yanayofanya kazi ambazo ni kinyume na maadili ya sheria za nchi," alisisitiza Salvatory.

Alisema mashirika yasiyo ya kiserikali yanatakiwa kuhakikisha mipango yao inalenga kutekeleza vipaumbele vya serikali iliyopo madarakani kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Vilevile, mashirika hayo yana wajibu wa kutekeleza Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 na kuhakikisha Amani, Umoja, Maendeleo na Utulivu vinakuwapo Mkoa wa Pwani.

Akisoma taarifa ya Utekelezaji wa Mashirika yasiyo ya kiserikali kwa niaba ya Msajili wa mashirika hayo, Grace Tete, alisema yaliyosajiliwa katika mkoa huo yanafanya kazi katika sekta ya afya, elimu, maji, miundombinu, sheria, utawala bora, haki za kibinadamu na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Tete alisema kwamba katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023, miradi 104 yenye thamani ya Sh. bilioni 2.8 imetekelezwa kwa wanufaika 55,759.

Pia, alisema utekelezaji wa miradi hiyo unachochea maendeleo ya kiuchumi na kuongeza kasi ya utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii katika mkoa wa Pwani.

# Tetemeko Morocco laathiri 300,000 vifo vya watu 2,000

**Marrakesh,** MOROCCO

TAKRIBANI watu 300,000 Mji wa Marrakesh na viunga vyake, wameathiriwa na tetemeko la ardhi, Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA) imesema.

Idadi ya waliofariki kwenye tetemeko hilo imeongezeka na kufikia zaidi ya watu 2,000 mwishoni mwa wiki. Wizara ya Mambo ya Ndani, ilisema zaidi ya watu 1,400 wamejeruhiwa vibaya na majeruhi wengi zaidi wako katika majimbo ya kusini mwa Marrakesh.

Mfalme Mohammed VI, alitangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa na kuamuru kupelekwa makazi ya muda, chakula na msaada mwingine kwa walionusurika.

Tetemeko hilo la kipimo cha 6.8 richta lilipiga Marrakesh na miji mingi, Ijumaa mwishoni mwa wiki majira ya usiku, huku maeneo ya mbali ya milimani, vijiji vinaripotiwa kusambaratika.

**Kutoka katika Milima ya Juu ya Atlas, 71km (maili 44) kusini-magharibi mwa Marrakesh, ambalo ni jiji lenye hadhi ya urithi wa dunia na maarufu kwa watalii.**

Kutoka katika Milima ya Juu ya Atlas, 71km (maili 44) kusini-magharibi mwa Marrakesh, ambalo ni jiji lenye hadhi ya urithi wa dunia na maarufu kwa watalii.

Lakini mitetemeko hiyo pia ilisikika katika mji mkuu wa Rabat, ulio umbali wa kilomita 350, pamoja na Casablanca, Agadir na Essaouira.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA), ilisema, inafuatilia kwa karibu hali hiyo na iko tayari kuunga mkono juhudi za uokoaji.

Katika taarifa ya awali, Umoja wa Mataifa (UN), ilisema iko tayari kuisaidia serikali ya Morocco katika juhudi zake za kuwasaidia watu walioathirika.

**WALIOATHIRIWA**

Aidha, mjini Marrakesh, maelfu ya watu wamekuwa wakitumia usiku wa tatu, kwenye maeneo ya wazi kulala. Maeneo ya mapumziko, maeneo ya kuegesha magari na viwanja vya umma vimejawa na idadi kubwa ya watu wa kila rika wakijilaza kwenye mablanketi.

Wachache wanaonekana kulala, wengi wako macho wakitafakari na kuhuzunika.

Kuna vifusi katika mitaa mingi ya Mji huo wa kihistoria, ingawa jiji hilo limekuwa na ahueni kuliko maeneo ya milimani kusini-magharibi.

Mmiliki wa mgahawa, Safa El Hakym, anajaribu kukubaliana na kilichotokea. Morocco iliwahi kushuhudia matetemeko makubwa ya ardhi hapo awali, ikiwa ni pamoja na mwaka wa 2004. Tetemeko la ardhi lilipiga al-Hoceima, kaskazini-mashariki mwa Morocco na kuua watu 628 na mwaka 1960, tetemeko la ardhi la Agadir, liliua watu 12,000.

Kitovu cha tetemeko la ardhi, kilikuwa katika Milima ya Atlas, kuliko na vijiji vingi vya mbali ambavyo ni vigumu kuvifikia. **BBC**



Mwonekano wa gari lililoathiriwa na tetemeko la ardhi lililoukumba Mji wa Marrakesh, nchini Morocco mwishoni mwa wiki. **PICHA: REUTER**

## Ethiopia yatimiza ahadi kujaza bwawa Mto Nile

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

ETHIOPIA imekamilisha awamu ya nne na ya mwisho ya kujaza maji kwenye bwawa kubwa lenye utata katika eneo la Blue Nile.

Tangazo hilo limetolewa jana, Jumapili, wiki kadhaa baada ya mazungumzo kati ya Addis Ababa na nchi mbili zinazonufaika na mto Nile, Misri na Sudan.

Mazungumzo yalianza tena kwa nia ya kutia saini makubaliano yenye nguvu ya kukabiliana na ukame katika siku zijazo. Duru mpya ya mazungumzo inatarajiwa kufanyika mwezi huu.

Bwawa la Grand Ethiopian Renaissance Dam (GERD), lenye thamani ya dola bilioni tano, limekuwa katikati ya mazungumzo ya kidiplomasia katika muongo mmoja uliopita, kati ya Ethiopia na nchi hizo mbili ambazo zinahofia upatikanaji muhimu wa maji kwao, kupitia mto Nile, kutishiwa au kuathiriwa na mradi huo.

Katika taarifa iliyochapishwa kwenye mtandao wa kijamii wa X (zamani wa Twitter).

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed alisifu kukamilika kwa ujazo huo kama hatua kubwa ambayo ilifanyika licha ya changamoto za ndani na shinikizo kutoka nje.

Habari hizo zinakuja huku kukiwa na ghasia zinazoendelea na kuongezeka kwa ukosefu wa usalama katika maeneo mengi Ethiopia, kwenye nchi ambayo bado inakabiliwa na makovu ya vita vya kikatili vya wenyewe kwa wenyewe vya miaka miwili, vilivyomalizika. **BBC**

## Mipango mazishi Buthelezi yaendelea

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

MAZISHI ya Mangosuthu Buthelezi, mwanasiasa mkongwe wa Afrika Kusini, mwanamfalme wa Kizulu na mtu mwenye utata wakati wa mapambano ya ukombozi wa ubaguzi wa rangi nchi hiyo, aliyefariki dunia mwishoni mwa wiki inaendelea kupangwa.

Ofisi ya Rais, ilisema amefariki akiwa na umri wa miaka 95. Mwasisi huyo wa chama cha Inkatha Freedom, alihudumu kwa mihula miwili kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi katika serikali ya baada ya ubaguzi wa rangi kumalizika na chama tawala cha African National Congress –ANC mwaka 1994 kuchukua utawala.

## Niger yaituhumu Ufaransa kupanga uvamizi

**Niamey,** NIGER

UTAWALA wa kijeshi wa Niger umeituhumu Ufaransa kwa kukusanya wanajeshi na vifaa katika mataifa jirani ya Afrika ya magharibi, kwa lengo la kuivamia kijeshi.

Akizungumza kupitia televisheni ya taifa mwishoni mwa wiki, Msemaji wa utawala huo, Kanali Amadou Abdramane, alisema Ufaransa inaendelea kupeleka vikosi vyake katika nchi kadhaa za Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika ya Magharibi (ECOWAS), ikiwa ni sehemu ya maandalizi kwa ajili ya uchokozi dhidi yake.

Alifafanua kwamba Ufaransa imeshapeleka ndege za kijeshi, helikopta na vifaru 40 katika nchi za Ivory Coast, Benin na Senegal.

Uhusiano kati ya Niger na koloni lake, Ufaransa, uliingia dosari baada ya Paris kusimama upande wa Rais aliyepinduliwa Julai, mwaka huu, Mohamed Bazoum na kusisitiza kutoutambua utawala wa kijeshi wa sasa. **DW**



Kanali Amadou Abdramane

# JKU YAPANIA KUKOLEZA MOTO NGAO YA JAMII LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

BAADA ya kutwaa Ngao ya Jamii juzi, Kocha Mkuu wa timu ya JKU, Salum Ali, amesema mwanzo mzuri waliouanza katika mchezo wao huo wa kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar 2023/24, wataendelea nao kwenye ligi hiyo inayotarajiwa kuanza rasmi Jumatano wiki hii.

JKU ilitwaa Ngao ya Jamii kwa kuifunga timu ya KMKM mabao 5-2 kwenye mchezo uliochezwa katika Dimba la Mau majira ya Saa kumi jioni juzi.

**Akizungumza na Nipashe jana, kocha huyo alisema mchezo wa Ngao ya Jamii kwao umeisha, hivyo wanajipanga kwa mechi za Ligi Kuu ambapo watashuka dimbani kwa mara ya kwanza msimu huu, Jumamosi wiki hii dhidi ya New City.**

Alisema kupitia mchezo huo wa Ngao ya Jamii, tayari amekijua kikosi chake namna gani atakavyokipanga ili kuhakikisha wanapata alama tatu katika mchezo huo wa kwanza kwao.

Aidha, kocha huyo alisema kuelekea michezo ya Ligi Kuu watakuwa makini na hawataidharau timu yoyote watakayocheza nayo kwani timu zote kwenye kinyang'anyiro hicho ni bora.

"Tumefanikiwa kushinda Ngao ya Jamii, kupitia mchezo huu umenipa mwanga na taswira ya kikosi changu kuelekea michezo ya Ligi Kuu, yapo makosa madogo madogo nimeyaona kwa wachezaji wangu, hivyo tutayafanyia kazi," alisema.

Alisema ili kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri zaidi, inapswa mashabiki wao kuendeleza hamasa na kuwa na shauku kama waliyoionesha katika mechi hiyo ya Ngao ya Jamii dhidi ya KMKM.

Alisema hamasa ya mashabiki inaweza kuwaamsha wachezaji kujituma na kuwa na hamu ya kufanya vema katika kila mchezo.

Hata hivyo, aliwapongeza wachezaji na uongozi wa timu hiyo kwa kufanikiwa kunyakuwa Ngao ya Jamii, lakini pia kwa kuhahamasisha mashabiki kwenda kwa wingi uwanjani.



Mkurugenzi wa Kampuni ya mbolea ya Yara Tanzania, Winstone Odhiambo (kushoto), akikabidhi zawadi kwa Twaha Juma wa Rotary Club Oysterbay, wakati wa Mbio za Mbuzi 2023, jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya kuchangia ufadhili wa elimu ya juu kwa wanafunzi wasiojiweza. Ufadhili wa Yara kwenye mbio hizo unaendana na malengo ya kampuni hiyo ya kukuza wanataaluma vijana hususan wanawake katika kilimo. **MPIGAPICHA WETU**

# TIC yaita wawekezaji sekta ya michezo

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji nchini (TIC), kimewataka wadau wa michezo kuchangamkia fursa zilizopo katika sekta ya michezo ili kukuza uwekezaji hali itakayosaidia kuongeza nafasi za ajira kwa vijana.

Kituo hicho kimesema iwapo idadi kubwa ya wawekezaji sekta ya michezo watajitokeza, watasaidia kuongeza kipato na kukuza mchango wa sekta hiyo katika ukuaji wa uchumi nchini.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es salaam na Mkurugenzi wa Idara ya Uhamasishaji Uwekezaji kutoka TIC, John Mnali, wakati akizungumza kwenye kikao kilichowakutanisha wadau mbalimbali wa michezo nchini.

Alisema TIC imepunguza gharama za uwekezaji kwa Watanzania na kufikia Dola za Marekani 50,000 ili kutoa fursa kwa wananchi wengi zaidi kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali nchini.

"Tunaposema Dola 50,000 kama mtaji wa kumwezesha kupata cheti cha uwekezaji, hatumaanishi kwamba lazima awe na fedha taslim, tunamaanisha thamani ya ardhi, thamani ya majengo, thamani ya magari na vitendea kazi vingine ambavyo amenunua," alisema Mnali

"Sekta ya michezo ina wadau wengi na inaajiri vijana wengi sana ndiyo sababu tumeona umuhimu wa kukaa na hawa wadau tuwaambie fursa zilizopo kwenye uwekezaji sekta ya michezo na kwa wale ambao tayari wameshawekeza namna wanavyoweza kupata vivutio wanapoamua kupanua uwekezaji wao," alisema Mnali

Alisema wawekezaji wanaotaka kuingia kuwekeza kwenye sekta ya michezo wajitokeze kwa wingi kwani wigo bado ni mpana na TIC imeweka vivutio vingi kwa wawekezaji wazawa tofauti na wageni.

Aliwaomba wawekezaji waliowekeza kwenye sekta hiyo wafike TIC kwa ajili ya kupewa vyeti vya uwekezaji ili waweze kunufaika na vivutio mbalimbali vya uwekezaji vinavyotolewa.

Naye Afisa Michezo Mwandamizi kutoka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Rashid Juza, alisema amefurahi kuona TIC ikihamasisha uwekezaji zaidi kwenye sekta hiyo ya michezo.

Alisema ni kweli sekta hiyo imesaidia maendeleo ya vijana wengi hivyo kuna umuhimu kwa wawekezaji wengi zaidi kujitokeza kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali ya michezo ili kusaidia vijana.

Naye Afisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Apansia Lema, alisema uwekezaji katika sekta hiyo utasaidia kuendeleza vipaji hivyo wataendelea kushirikiana na TIC kuwajengea uwezo wadau wa michezo nchini ili wawekeze katika vituo vya michezo.

## Uhuru aibukia Stand United

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa zamani wa Klabu ya Simba, Uhuru Selemani (pichani), ameibukia Stand United akisajiliwa kuichezea timu hiyo katika Ligi ya Championship iliyoanza jana nchini.

Mbali na mchezaji huyo, klabu hiyo pia imemtambulisha kocha mpya, Zulfikir Idd Mahdi, ambaye ndiye atakuwa mkuu wa benchi la ufundi.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imesema usajili wa Uhuru ni wenye tija kwani ni mchezaji mzoefu ambaye amecheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mafanikio na yeye ndiye anayewaongoza wenzake kuelekea kwenye njia hiyo.

"Tunayo furaha kumtambulisha kwenu wanachana na mashabiki wa Stand United mchezaji mwenye uzoefu mkubwa katika ngazi ya kitaifa hadi kimataifa, Uhuru Selemani, tunaamini uzoefu wake utakuwa chachu ya kuwapa furaha mashabiki wetu, pia tunayo furaha kuwatambulisha Kocha Mkuu atakayeongoza benchi la ufundi msimu huu, Zulfikir Idd Mahdi," ilieleza taarifa hiyo.



## Mbeya City hasira zote Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya City ambayo ilishuka daraja msimu huu kutoka Ligi Kuu Tanzania Bara, juzi ilianza Ligi ya Championship kwa hasira, ilipotembeza kichapo cha mabao 5-2 dhidi ya Green Warriors.

Wakati Mbeya City ikianza vema, timu nyingine iliyoshuka daraja msimu huu, Polisi Tanzania ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya Kwanza ambayo ilishuka daraja msimu wa 2021/22.

Ikichezwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, Sokoine jijini Mbeya, Mbeya City ilianza biashara ya kutaka kurudi Ligi Kuu asubuhi ilipoipa kichapo cha mabao 5-2 maafande wa Green Warriors katika moja kati ya mechi za ufunguzi wa ligi hiyo.

Mechi nyingine ya ufunguzi ilikuwa kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara wakati Mbeya Kwanza iliyoamua kuutumia uwanja huo ilipolamimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania. Mabingwa wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1982, Pan African nao walianza vema ligi hiyo wakiwa ugenini, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza kwa kuichapa Copco mabao 3-2.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### SANCHO KUREJEA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inapanga kumrejesha, Jadon Sancho, 23, katika dirisha la Januari kama winga huyo wa Manchester United atashindwa kumshawishi kocha, Erik ten Hag. ***(Sun)***

#### ODEGAARD MKATABA MPYA

KLABU ya Arsenal inapanga kuendelea na mazungumzo na kiungo wa kati wa Norway, Martin Odegaard, 24, kuhusu mkataba mpya kuendelea kusalia katika klabu hiyo. ***(Fabrizio Romano)***

#### ALVAREZ ATAKIWA MADRID

KLABU ya Real Madrid ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Julian Alvarez, 23, kutoka Manchester City. ***(Fichajes, vi Goal)***

#### MOS SALAH AKOMALIWA

MKURUGENZI wa Soka wa Ligi ya Saudi Arabia (Saudi Pro League), Michael Emenalo, amesema ligi hiyo "haitafunga milango" katika harakati zake za kumsaka winga wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah, 31. ***(Sky Sports)***

#### RICHARLISON NA WASAUDIA

KLABU ya Al-Ittihad ilimfuatilia mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na Brazil, Richarlison kama mbadala wa Mohamed Salah baada ya dau lao la pauni milioni 150 kwa ajili ya mshambuliaji huyo wa Liverpool kukataliwa. ***(Telegraph)***

#### DODRI ATAKA UDHIBITI

KIUNGO wa kati wa Manchester City na Hispania, Rodri, 27, amesema mamlaka ya soka inahitaji kudhibiti uhamisho wa wachezaji kwenda Saudi Pro League. ***(Sky Sport)***

#### CHELSEA YASAKA NYOTA

CHELSEA inatafuta kuimarisha chaguo lao la mshambuliaji wa kati katika dirisha la usajili la Januari huku washambuliaji wawili wa England, Ivan Toney, 27 na Ollie Watkins wa Aston Villa - na mshambuliaji wa RB Leipzig na Slovenia, Benjamin Sesko, 20, wakiwa kwenye orodha ya wanaosakwa. ***(Givemesport)***

#### BALDE KAULIZIWA CITY

KLABU ya Manchester City iliulizia kuhusu mlinzi wa Barcelona na Hispania, Alejandro Balde, 19, mapema msimu huu wa majira ya joto, lakini hawakutoa ofa, wakati huu akijiandaa kusaini mkataba mpya hadi 2028. ***(Fabrizio Romano).***

#### DRAXLER, AL-AHLI WAMALIZA

KIUNGO wa kati wa Paris Saint-Germain na Ujerumani, Julian Draxler, 29, amekubali kujiunga na Klabu ya Qatar Al-Ahli SC ***(Hadrien Grenier)***

#### SCHAR AFUNGWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United itaanzisha mazungumzo na mlinzi wa Uswisi, Fabian Schar, 31, kuhusu mkataba mpya pale St James' Park. ***(Football Insider)***

#### ENDRE AWINDWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inapanga kumnunua kiungo wa Fluminense na Brazil, Andre, 20, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(ESPN, via Football 365)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOUTHGATE AWABWATUKIA WASHAMBULIAJI ENGLAND

**WROCLAW,** Poland

**Tuligeuza na kupoteza mipira mingi sana ambayo haikuwa kawaida, sitarajii...**

GARETH Southgate aliwajia juu washambuliaji wake kwa kuwaambia hawakuonesha kiwango kizuri katika sare ya England ya bao 1-1 dhidi ya Ukraine katika mchezo wa kufuzu Euro 2024 na akawaonya hatarajii kuona tena uzembe kama huo.

**Kuanzia kwa James Maddison, Bukayo Saka na Harry Kane, huku Jude Bellingham pia akijiunga na safu ya ushambuliaji, Southgate alikiri kwamba England ilikuwa butu kwa viwango vyao vya washambuliaji wake, ikilinganishwa katika mechi za ushindi dhidi ya Italia, Macedonia Kaskazini na Malta.**

Southgate alisema: "Ni wazi, sehemu kubwa ya wachezaji wetu wa safu ya ushambuliaji hawakuwa katika kiwango ambacho tulikitarajia.

"Nadhani kufikia wakati tunafunga bao tulikuwa tumepata zaidi ya asilimia 70 ya mpira, lakini hilo lilikuwa jaribio letu la kwanza kulenga goli.

"Tuligeuza na kupoteza mipira mingi sana ambayo haikuwa kawaida. Sitarajii hili kutokea tena.

"Tunajua kuwa mifumo ambayo tulifanya kazi kwa wiki ndiyo tunayofanya kila wakati, kwa hiyo si kwamba tunachukulia mchezo kwa njia tofauti.

"Tulijaribu kuibua upya mambo ili kuwapa tatizo la aina tofauti lakini leo (juzi) uchezaji wetu wa mbele, kuzuia goli na juhudi za Bukayo Saka hazikuwa katika kiwango ambacho kimekuwa katika michezo yetu ya awali."

Hata hivyo, Southgate alibainisha kuwa amefurahishwa na hatua hiyo, huku England ikiwa bado iko mbioni kufuzu kwa Euro 2024 na timu ikirejea katika hali ya ushabiki mkali, huku Waukraine 45,000 wakiwa uhamishoni walijaza Uwanja wa Tarczynski Arena huko Wroclaw kusini mwa Poland.

Southgate alisema: "Ukweli ni kwamba hatutashinda kila mechi kwa nne au saba kama tulivyofanya katika kampeni hii ya kufuzu. Huo ulikuwa mtihani mzuri sana, mbali na nyumbani, hali ya shauku ni kubwa sana.

"Ni hatua muhimu sana kwetu na sasa tumecheza na timu mbili zilizoorodheshwa bora ugenini na tumepata pointi nne kutokana na michezo hiyo miwili.

"Nilichopenda ni udhibiti wa mchezo ambao tulikuwa nao unapoingia kwenye hali ya hewa kali kama ilivyokuwa.

"Nilidhani tulicheza kwa utulivu wa kweli hadi theluthi ya mwisho kwa kuzingatia mazingira na umuhimu wa uhakika katika suala la kufuzu na kutoka nyuma wakati umati wa watu umejaa na wapinzani wana kitu cha kushikilia."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
PORTUGAL
VERSUS
LUXEMBOURG
1 | 1.13
X | 7.56
2 | 22.85

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARSENAL YASITISHA MKATABA NA PEPE



**LONDON,** England

ARSENAL ilisitisha mkataba wa mchezaji aliyesajiliwa kwa rekodi ya zamani ya klabu hiyo, Nicolas Pepe juzi na kumwachia winga huyo kuondoka bila malipo.

Arsenal ililipa pauni milioni 72 kumsajili Pepe kutoka Klabu ya Lille ya Ufaransa mwaka 2019, lakini hawatapata chochote kwa kuondoka kwake, huku mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ivory Coast akiripotiwa kusajiliwa na Trabzonspor ya Uturuki.

Pepe alikuwa na mwanzo mzuri Arsenal chini ya kocha wa zamani, Unai Emery, lakini alijitahidi kuwa juu baada ya Mikel Arteta kuchukua mikoba, na hajaanza mechi ya Ligi Kuu tangu Oktoba 2021.

Alipelekwa Nice kwa mkopo msimu uliopita, na alikuwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake, lakini Arsenal waliamua kumwachia badala ya kumtumia kama mbadala wa Bukayo Saka pale Emirates.

"Kila mtu Arsenal anamshukuru Nicolas kwa mchango wake wakati akiwa nasi na tunamtakia heri kwa siku zijazo," taarifa ya klabu hiyo ya London ilisema katika taarifa yake.



## Flick akalia kuti kavu Ujerumar

**WOLFSBURG,** Ujerumani

KOCHA wa Ujerumani, Hansi Flick, amesema yeye bado ni mtu sahihi kuiongoza timu hiyo licha ya kufungwa mabao 4-1 nyumbani dhidi ya Japan katika mechi ya kirafiki ya kimataifa Jumamosi, pamoja na kuwapo shinikizo kubwa kutokana na msururu wa matokeo mabaya.

Ujerumani, mabingwa mara nne wa dunia, ilikuwa na matumaini kwamba mechi hiyo ingeashiria mwanzo mpya kwao miezi tisa kabla ya kuandaa michuano ya Euro 2024.

Badala yake iligeuka kuwa mzozo na kupoteza kwao kwa mara ya tatu mfululizo huku kukiwa na kejeli na filimbi kutoka kwa mashabiki wa nyumbani.

Flick alikuwa tayari akishutumiwa kabla ya mechi hiyo huku timu yake ikiwa imeshinda mechi nne pekee kati ya 16 zilizopita kabla ya Jumamosi na kutolewa katika raundi ya kwanza ya Kombe la Dunia mwaka jana.

Kuteleza kwao kwa
sasa kutasababisha uw
kano wa Flick kutimuliwa

"Najua katika soka k
mabadiliko na siwezi kuta
kitakachotokea, lakini kut
upande wangu tunaja
kila kitu kuandaa timu
zuri," alisema Flick akiwa
bia waandishi wa habari.

"Nadhani tunafanya
nzuri na nadhani mimi n
mtu sahihi kwa kazi hi
alisema alipoulizwa kuh
mustakabali wake.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# MAYELE AIPELEKA DRC AFCON

**KINSHASA,** DR Congo

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Yanga SC, Fiston Mayele aliiwezesha nchi yake ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kufuzu kucheza michuano ya Afcon 2023, baada ya kufunga bao la pili dhidi ya Sudan, juzi Jumamosi.

Mayele ambaye aliondoka Yanga na kujiunga na Pyramids ya Misri majira haya ya joto, alifunga bao hilo dakika ya 87 likiwa ni la pili kwa kikosi hicho kwenye mchezo huo ambao waliibuka na ushindi wa mabao 2-0.

> **Kabla ya Mayele kuihakikishia ushindi DR Congo, mchezaji Theo Bongoda aliiweka mbele kwa bao la mapema la dakika ya nane.**

Ushindi huo umeifanya DR Congo kumaliza ukame wa miaka 56 wa kutoshinda dhidi Sudan kwenye michuano hiyo.

Pia ushindi huo unamaanisha kwamba, DR Congo imefikisha poonti 12 katika kundi lake la I ikiongoza msimamo na imefuzu kwa michuano hiyo itakayoanza kutimua vumbi Januari 13, mwakani nchini Ivory Coast.



Ikiwa imeshiriki michuao hiyo mara 19, DR Congo ina historia ya kulitwaa taji hilo mara mbili, mwaka 1968 na 1974. Katika kundi hilo la I pia kuna timu za Mauritania, Gabon na Sudan.

Mauritania inashika nafasi ya pili kwenye kundi ikiwa na pointi 10, ikifuatiwa na Gabon yenye pointi 7 iliyopo kwenye nafasi tatu, huku nafasi ya nne ikishikwa na Sudan yenye alama sita.




Msanii wa Muziki wa Kizazi kipya na Balozi wa Airtel, Diamond Platnumz (wa pili kulia), akipozi kwa picha na mmoja wa wakazi wa Ruangwa aliyemsajilia laini yake ya Airtel muda mfupi baada ya kuzindua rasmi duka la Airtel Money (Airtel Money Branch), mjini Ruangwa, Lindi mwishoni mwa wiki. Kushoto kwake ni msanii, Khery Sameer Rajabu 'Mr Blue' na wa kwanza kushoto ni Meneja Mauzo wa Airtel Lindi, Salehe Safi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Yanga yaahidi tena rekodi CAF

INATOKA UKURASA 24

mkakati wa kuhakikisha inatinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa baada ya kutoweza kufanya hivyo kwa miaka 24 sasa.

Mara ya mwisho kutinga hatua hiyo ilikuwa ni 1998 ilipoifunga Coffee SC ya Ethiopia jumla ya mabao 8-3, zikitoka sare ya mabao 2-2 nchini Ethiopia, kabla ya Yanga kushinda nchini mabao 6-1 katika mechi ya marudiano, ikiwa ni raundi ya pili ya michuano hiyo.

## *Kramo amuibua Robertinho kwa Power Dynamos*

INATOKA UKURASA 24

kidogo kwenye mechi ya leo (juzi), ninaimani atakuwa sawa baada ya vipimo vya daktari, " alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa anaimani watakuwa imara zaidi kuelekea mechi yao ya dhidi ya Power Dynamos kwa kuhakikisha wanaenda kutafuta ushindi ndani ya dakika 90 ugenini.

Kocha huyo alisema mechi zote mbili ni muhimu na nafasi ya kipekee kabisa kuhakikisha wanashinda ili kusonga mbele kucheza hatua ya makundi baadaye robo na hatimaye kuitaka nusu fainali.

"Simba ni timu kubwa ninaimani kubwa na wachezaji wangu kufikia malengo yetu, naendelea kuwasisitizia kuwa licha ya Power Dynamos kuwafunga katika mechi yetu ya kirafiki lakini safari hii watakuja kivingine na tunahitaji kucheza kwa kuwaheshimu wanapokuwa kwao na kutaka kutumia nafasi zinazopatikana," alisema Robertinho.


## MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 11/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2800 | Crewe U21 vs Watford U21 | 2.27 | 3.78 | 2.54 |
| 16:00 | 3087 | Birmingham U21 vs Millwall U21 | 4.18 | 4.48 | 1.57 |
| 16:30 | 4015 | Arsenal Tula vs FK Khimki | 2.83 | 3.09 | 2.31 |
| 17:00 | 4761 | AL Tora vs Al-Arabi | 3.35 | 3.15 | 2.00 |
| 17:00 | 5783 | Sama AL Sarhan vs Jazeera Amman | 3.04 | 3.29 | 2.14 |
| 17:15 | 4491 | Poland U20 vs Germany U20 | 2.80 | 3.31 | 2.26 |
| 18:00 | 4953 | Al-Yarmouk vs DAR AL Dawa | 2.49 | 3.35 | 2.50 |
| 18:00 | 5759 | Estudiantes de La Plata vs CA Banfield | 2.55 | 2.95 | 2.55 |
| 18:30 | 4933 | Esteghlal Mollasani vs Chador Malu Yazd | 2.60 | 2.60 | 3.01 |
| 19:00 | 1143 | Egypt U23 vs Russia | 3.11 | 3.17 | 2.36 |
| 19:00 | 1938 | Denmark U21 vs Slovakia U21 | 1.55 | 4.02 | 4.88 |
| 19:00 | 2679 | Luxembourg U21 vs England U21 | 35.59 | 10.17 | 1.03 |
| 19:00 | 2790 | Maccabi Jaffa vs Hapoel Ramat Gan | 1.95 | 3.31 | 3.78 |
| 19:00 | 3315 | Guinea Bissau vs Sierra Leone | 1.82 | 3.37 | 4.25 |
| 19:00 | 3735 | Ironi Kiryat Shmona vs Bnei Yehuda | 1.97 | 3.51 | 3.46 |
| 19:00 | 3959 | Slovenia U21 vs France U21 | 6.30 | 4.47 | 1.39 |
| 19:00 | 4494 | Fredrikstad FK 2 vs Start 2 | 2.15 | 3.90 | 2.58 |
| 19:00 | 4558 | Ihud Bnei Shfaram vs Nazareth Ilit | 4.35 | 3.68 | 1.73 |
| 19:00 | 5379 | Armenia vs Croatia | 7.25 | 4.32 | 1.45 |
| 19:30 | 2309 | Stomil Olsztyn vs KKS 1925 Kalisz | 2.39 | 3.21 | 2.70 |
| 19:30 | 3665 | Torpedo Moscow vs Akron Tolyatti | 2.19 | 3.13 | 2.98 |
| 20:00 | 2028 | Skeid Fotball 2 vs Sarpsborg Sparta 2 | 1.62 | 4.34 | 3.78 |
| 20:00 | 4790 | Mjondalen 2 vs Sandefjord Fotball 2 | 2.31 | 3.94 | 2.37 |
| 20:00 | 5736 | FC Trollhattan vs IK Oddevold | 2.35 | 3.28 | 2.63 |
| 20:30 | 5262 | Red Star vs FC Rouen | 1.78 | 3.41 | 4.35 |
| 21:00 | 3024 | Reading U21 vs Blackburn Rovers U23 | 1.94 | 3.72 | 3.16 |
| 21:00 | 3409 | Belgium U21 vs Kazakhstan U21 | 1.06 | 8.96 | 22.41 |
| 21:00 | 4255 | Deportivo Coopsol vs Molinos EL Pirata FC | 1.27 | 4.85 | 8.48 |
| 21:10 | 4805 | Boca Juniors vs Ferro Carril Oeste | 1.10 | 6.80 | 17.00 |
| 21:30 | 1272 | General Lamadrid vs Victoriano Arenas | 1.49 | 3.60 | 5.80 |
| 21:30 | 2154 | Berazategui vs Claypole | 2.75 | 2.80 | 2.50 |
| 21:30 | 2423 | Central Cordoba vs CA Atlas | 2.10 | 2.85 | 3.40 |
| 21:30 | 3003 | CA Fenix vs Deportivo Merlo | 1.97 | 3.05 | 3.76 |
| 21:30 | 3308 | Wisla Pulawy vs Polonia Bytom SA | 1.66 | 3.66 | 4.47 |
| 21:40 | 4730 | Nueva Chicago vs Patronato Parana | 2.20 | 2.90 | 3.34 |
| 21:45 | 1751 | Hitchin Town vs Nuneaton | 2.38 | 3.65 | 2.36 |
| 21:45 | 2256 | Latvia vs Wales | 6.53 | 4.11 | 1.51 |
| 21:45 | 2503 | AZ Picerno vs Taranto Sport | 2.06 | 3.09 | 3.82 |
| 21:45 | 3307 | Juve Stabia vs Avellino | 2.42 | 3.04 | 3.04 |
| 21:45 | 3835 | Slovakia vs Liechtenstein | 1.07 | 9.48 | 42.13 |
| 21:45 | 4467 | Foggia vs FC Giugliano 1928 | 1.97 | 3.30 | 3.87 |
| 21:45 | 4835 | Iceland vs Bosnia and Herzegovina | 3.11 | 3.17 | 2.36 |
| 21:45 | 5462 | Portugal vs Luxembourg | 1.13 | 7.56 | 22.85 |
| 21:45 | 5812 | Benevento vs Virtus Francavilla | 1.77 | 3.55 | 4.49 |
| 22:00 | 3349 | Spain U21 vs Scotland U21 | 1.21 | 5.90 | 9.56 |
| 22:00 | 3430 | Orleans vs Le Mans | 2.44 | 3.21 | 2.74 |
| 22:00 | 4405 | CD Eldense vs Alcorcon | 2.27 | 2.92 | 3.27 |
| 23:00 | 2564 | Universitario Popayan vs Llaneros FC | 2.32 | 3.10 | 2.89 |
| 23:00 | 3303 | Patriotas FC vs FC Aguablanca | 1.44 | 4.07 | 6.32 |
| 23:30 | 5047 | Cayman Islands vs Aruba | 3.27 | 3.27 | 2.05 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Septemba 11, 2023
Nipashe



Mayele aipeleka DRC AFCON UKURASA 23



Wachezaji wa Simba, Aubin Kramo (jezi namba 24) na Israel Mwenda (Jezi namba 5), wakishangaa namna Luis Miquissone, alivyobinjuka kuucheza mpira katika mazoezi ya timu hiyo yanayoendelea Uwanja wa Simba Mo Arena uliopo Bunju, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yaahidi tena rekodi CAF

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikijiandaa kuondoka nchini Alhamisi ijayo kwenda Kigali nchini Rwanda kwa ajili ya mechi ya mkondo wa kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan, Klabu ya Yanga imetamba kutaka kuweka rekodi nyingine ambayo haijawahi kuwekwa hapa nchini, kwani wachezaji wake wana njaa ya mafanikio.

Makamu Rais wa Klabu hiyo, Arafat Haji, amesema juzi kuwa, moja kati ya siri ya mafanikio ni pamoja na usajili mzuri walioufanya, lakini pia wachezaji wa timu hiyo wanaonekana wana njaa kubwa ya kupata mafanikio kwa ajili ya kuipa heshima na sifa klabu, pia maisha yao ya baadaye kisoka.

Jumamosi ijayo, Yanga itacheza mchezo wa raundi ya kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika na timu hiyo kwenye Uwanja wa Pele, Nyamirambo nchini Rwanda.

"Tuna kikosi kizuri na tuna wachezaji ambao wana uzoefu kwenye mashindano haya ya Afrika, na tuna kikosi ambacho wachezaji wake wana njaa ya mafanikio na wanataka kuwa alama ya mafanikio katika klabu yetu, wanachama na mashabiki wasiwe na mashaka, wajiandae kuendelea kushangilia matokeo mazuri ambayo waliyaona msimu uliopita, msimu uliopita ilikuwa Kombe la Shirikisho, lakini safari hii yakihamia Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Arafat.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kusafiri kwa wingi kwenda kuwapa sapoti wachezaji wao na kupata burudani ambayo wameikosa kwa wiki mbili sasa.

"Watakwenda kupata burudani ambayo wameikosa kwa wiki mbili sasa baada ya kikosi chao kutoonekana uwanjani, nawaambia wanachama na mashabiki kuwa tunakwenda kufanya kazi nzuri Kigali ambayo itatuhakikishia kuendelea na safari ya kutembea katika bara la Afrika, nia ni kuweka rekodi nyingine kwenye Ligi ya Mabingwa ambayo haijawahi kuwekwa na timu yoyote Tanzania," alisema.

Yanga iko kwenye

INAENDELEA UKURASA 23

# Kramo amuibua Robertinho

### ●●● Azitaka dakika 90 za Power Dynamos Zambia, huku akiwaonya wachezaji Simba...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kucheza mechi tatu za kujipima na kupata muunganiko wa wachezaji wake, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliviera, ameridhishwa na nyota wake, Aubin Kramo kwa kufanya kazi nzuri na kufunga mechi za kirafiki tangu aliporejea uwanjani akitokea chumba cha majeruhi.

Kramo aliyesajiliwa na Simba akitokea ASEC Mimosas ya Ivory Coast, hajaonesha makeke yake uwanjani kutokana na kusumbuliwa na majeraha wakati wamaandalizi ya Ngao ya Jamii, Mkwakwani jijini Tanga, lakini sasa amerejea kwa kasi katika mechi za kirafiki na kugusa 'mtima' wa kocha huyo.

**Simba inaendelea kujiandaa na mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos itakayopigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Levy Mwanawasa nchini Zambia kabla ya kurudiana Oktoba 29, mwaka huu jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema wachezaji wote wapo tayari kwa mechi zilizopo mbele yao ikiwa ni zile za ligi, African Football League (AFL), na Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos.

Alisema Kramo alikosa mechi ambazo timu hiyo ilicheza kwa kuwa alikuwa bado hajawa fiti, lakini sasa taratibu anazidi kuwa imara kutokana na kile anachokionesha mazoezini na kufunga katika mechi zote za kirafiki.

"Tumefanya maandalizi mazuri, nimeridhishwa na kazi nzuri, matumaini yangu ni kufanya vizuri kwenye mechi yetu dhidi ya Power Dynamos, Kramo amerudi vizuri licha ya kupata shida

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >